# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ILIYOSOMWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI NA WAZIRI WA NCHI, AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS MHESHIMIWA HARUSI SAID SULEIMAN (MBM)

**MEI, 2025**



Mheshimiwa Othman Masoud Othman
Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar



Ndg. Maryam Juma Abdalla
Katibu Mkuu
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais  Zanzibar



Mheshimiwa Harusi Said Suleiman
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar



Kanali Burhani Z. Nassoro
Kamishna Mkuu,
Mamlaka ya Kudhibiti
na Kupambana na
Dawa za Kulevya



Ndg. Sheha Mjaja Juma
Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Usimamizi
wa Mazingira



Dkt. Ahmed M. Khatib
Mkurugenzi Mtendaji
Tume ya UKIMWI
Zanzibar



Mhandisi Ussy Khamis Debe
Katibu Mtendaji
Baraza la Taifa la Watu
wenye Ulemavu



Ndg. Ahmed Abubakar
Afisa Mdhamin



Ndg. Juma Ali Simai
Mkurugenzi Uendeshaji
na Utumishi



Ndg. Ilyasa P. Haji
Mkurugenzi Mipango,
Sera na Utafiti



Ndg. Farhat Ali Mbarouk
Mkurugenzi Idara ya
Mazingira



Ndg. Issa Kheri Hussein
Katibu wa
Makamu wa Kwanza
wa Rais Zanzibar

# YALIYOMO

YALIYOMO ........................................................................ iii

VIFUPISHO VYA MANENO ................................................ iv

UTANGULIZI ...................................................................... 1

MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA ............................... 5

MIKAKATI YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. ................................ 7

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE 2020-2024 ................................................ 8

UKUZAJI WA HUDUMA KWA JAMII KATIKA UJENZI WA UCHUMI IMARA NA SALAMA, SHIRIKISHI, ENDELEVU NA HIMILIVU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ............ 19

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025...... 23

MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ........................................................................ 26

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. ...................................................................... 28

CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA .................. 34

UTEKELEZAJI WA MALENGO KUPITIA PROGRAMU ZA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA KWA RAIS KUANZIA JULAI 2024 – MACHI 2025. ........................................ 38

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .......... 72
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KWAKA WA FEDHA WA 2025/2026. .......... 75
MALENGO YA PROGRAMU ZA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 . .......... 76
SHUKRANI .......... 91
VIAMBATANISHO .......... 94

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| AYAHIZA | - | Asociation of Young People Against HIV and AIDS Zanzibar |
| BSAAT | - | Building Sustainable Anti corruption Action in Tanzania |
| CBID | - | Communit Based Inclusive Development |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CCTV | - | Closed Circuit Television |
| CFP | - | Community Forest Program |
| COFMA | - | Community Forest Management Areas |
| COSTECH | - | Tanzania Commision for Science and Technology |
| DCEA | - | Drug Control and Enforcement Authority |
| DEA | - | Drug Enforcement Authority |
| DPP | - | Director of Public Prosecution |
| EBARR Rural | - | Eco System Based Adaptation for Resilience |
| ESA | - | European Space Agency |
| GST | - | Goods and Service Tax |
| ICT | - | Information and Communication Technology |

| | | |
|---|---|---|
| ILO | - | International Labour Organization |
| IPA | - | Institute of Public Administration |
| JKU | - | Jeshi la Kukuza Uchumi |
| KIST | - | Karume Institute of Science and Technology |
| KMKM | - | Kikosi maalum cha Kuzuia Magendo |
| KOICA | - | Korea Internation Co |
| KVZ | - | Kikosi cha Valantia Zanzibar |
| MoU | - | Memorandom of Understandings |
| NAP | - | National Adaptation Program |
| NCA | - | National Construction Authority |
| OMKR | - | Ofisi ya Mkamu wa Kwanza wa Rais |
| PBB | - | Program Based Budgeting |
| PBZ | - | People Bank of Zanzibar |
| PECCA | - | Pemba Chanel Conservation Areas |
| PGD | - | Post Graduate Diploma |
| PrEP | - | Pre – exposure Prophylaxis |
| SACCOS | - | Savings and Cradit Co operative Society |
| SAPPHIRE | - | Strategic Action Program Policy Hamonization and Instituional Reform |
| SDGs | - | Sectoral Development Goals |

| | | |
|---|---|---|
| SHIJUWAZA | - | Shirikisho la Jumuia za Watu wenye Ulemavu |
| SMZ | - | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TV | - | Television |
| TBC | - | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| TEHAMA | - | Taknologia ya Habari na Mawasiliano |
| TRA | - | Tanzania Revenue Authority |
| TZS | - | Tanzania Shilings |
| UK | - | United Kingdom |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UMATI | - | Chama cha Uzazi na Malezi bora Tanzania |
| UNAIDS | - | United Nations Agency for International Development |
| UNDP | - | United Nation Development Program |
| UNDP | - | United Nation Development Program |
| UNEP | - | United Nation Environmental Program |
| UNODC | - | United Nations Office for Drugs and Crime |

| | | |
|---|---|---|
| UPEPG | - | Uzi Island Planting mangroves and Environmental Protection Group |
| VVU | - | Virus Vya UKIMWI |
| ZADEP | - | Zanzibar Development Plan |
| ZEEA | - | Zanzibar Economic Empowerment Agency |
| ZANGOC | - | Zanzibar NGOs Cluster for HIV/ AID Prevention |
| ZAYEDESA | - | Zanzibar Youth Education, Environmental Suport Association |
| ZBC | - | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| ZBS | - | Zanzibar Bureau of Standard |
| ZCTV | - | Zanzibar Cable Television |
| ZDCEA | - | Zanzibar Drug Control and Enforcement Authority |
| ZGAMIS | - | Zanzibar Government Management Information System |
| ZYF | - | Zanzibar Youth Forum |
| ZPDB | - | Zanzibar Presidential Delivery Bureau |

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA FEDHA WA 2025/2026.

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili iweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

2. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima na afya njema pamoja na kuibariki Nchi yetu kuendelea kuwa na amani, Umoja na Mshikamano. Ni dhahiri kwamba hali hiyo imezidi kuimarika chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi ambae amekuwa akisisitiza umuhimu wa kudumisha amani kila anapokutana na viongozi mbalimbali wa Serikali, vyama, Kidini na wananchi. Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, busara na uwezo zaidi wa kuiongoza Zanzibar na kuleta maendeleo makubwa.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali

Mwinyi kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu tangu achaguliwe na wananchi kushika dhamana ya kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha 2020/2025 chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, pamoja na kudumisha amani, utulivu na mshikamano hali ambayo imepelekea kupata maendeleo makubwa katika sekta zote nchini na kuweza kukuza pato la Taifa kutoka asilima 5.1 kwa mwaka 2021 hadi 7.1 kwa mwaka 2024 na hatimae kuendelea kutambulika kama ni nchi yenye uchumi wa kati (middle income).

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020/2025, Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kupelekea kuteuliwa tena na Chama Cha Mapinduzi kugombea kwa mara ya pili nafasi ya urais wa Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2025/2030. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu, afya, hekima na busara ili aweze kufikia azma na tunu yake ya kuwaletea maendeleo zaidi wananchi wa Zanzibar.

5. **Mheshimiwa Spika,** shukrani za pekee ziende kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan kwa umahiri wake wa kuiongoza vyema Tanzania na kuimarisha mashirikiano makubwa na Rais wa Zanzibar na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi na hatimae kustawisha Muungano wetu kwa kuendelea kuimarisha amani na utulivu nchini. Aidha, jitihada zao za kukuza mashirikiano ya Kidiplomasia, Kubuni na kuendeleza miradi mipya ya maendeleo katika sekta mbali mbali zimesaidia sana katika utoaji wa huduma, kuimarisha ustawi wa jamii, ukuwaji wa demokrasia na uchumi wa Taifa letu.

6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa natumia nafasi hii kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuendelea kumshauri vyema Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuimarisha mshikamano na kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambapo tunakiri kwamba tumepata mafanikio makubwa. Pia, nampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa kutekeleza majukumu ya Taifa kwa ufanisi mkubwa akiwa ni msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara, siha njema, mashirikiano na mshikamano katika kuimarisha ustawi wa jamii na maendeleo ya Taifa letu.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia nafasi hii nikupongeze wewe binafsi kwa namna unavyoliongoza Baraza la Wawakilishi ambalo limekuwa tulivu na

kufanya Wajumbe wa Baraza kuwa huru, kuchangia hoja na kutoa mawazo yao pasi na vikwazo kwa muda wote wa vikao vya Baraza. Aidha, nampongeza Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi ikiwemo Kamati ya Bajeti na Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo za Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna wanavyotoa hoja na michango iliyopelekea kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa watendaji wa Taasisi na Idara mbalimbali na kurahisisha maendeleo ya nchi, namuomba Mwenyezi mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na Busara.

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Machano Othman Said Mwakilishi wa wananchi jimbo la Mfenesini pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Makatibu chini ya uongozi wake mahiri na namna anavyoendesha na kusimamia kwa umakini kazi za kamati. Aidha, naomba nikiri kwamba ushirikiano, michango na maelekezo yeo yamekuwa ni chachu kubwa ya kuleta mabadiliko chanya ya kiutendaji yaliyopelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika Afisi yetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia niwashukuru wananchi wa jimbo la Wete Pemba kwa kuendelea

kuniamini pamoja na kuniunga mkono katika kazi zangu za uwaziri na Uwakilishi hadi leo. Naomba niwaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta maendeleo jimboni. Mwisho kabisa naomba niishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu wao mkubwa na mashirikiano wanayonipa muda wote wa kutekeleza majukumu ya Kitaifa. Kwa dhati kabisa, nawashukuru watendaji wote wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipatia. Nikiri kuwa, mashirikiano hayo yamekuwa yakirahisisha sana na kunipa moyo katika kufanya kazi za utekelezaji wa majukumu tuliyopangiwa kwa ufanisi mkubwa.

## A. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jumla ya wafanyakazi 391 kwa Unguja na Pemba, ambapo wanaume ni 209 na wanawake ni 182 na imeundwa kwa Idara Nne (4), Taasisi Nne (4) na Afisi Kuu Pemba Pamoja na bodi nne ambazo zinazosimamia Taasisi kama ifuatavyo:

**Idara:**

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
3. Idara ya Faragha,
4. Idara ya Mazingira,
5. Afisi Kuu Pemba

**Taasisi:**

1. Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira,
2. Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu,
3. Tume ya Taifa ya UKIMWI,
4. Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,

**Bodi za Afisi:**

1. Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira,
2. Bodi ya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu,
3. Bodi ya Tume ya Taifa ya UKIMWI,
4. Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

11. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kusimamia maeneo makuu manne ya kiutekelezaji ambayo ni usimamizi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, kusimamia masuala yanayohusu Watu wenye Ulemavu, udhibiti na kupambana na dawa za kulevya pamoja na mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI. Aidha, dhamira hii imefikiwa na imetekelezwa kwa kuimarisha sekta zote zinazosimamia kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Mpango Mkuu wa maendeleo wa Taifa (ZADEP 2021/2026), Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020/2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mikataba ya kimataifa, Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo.

## B. MIKAKATI YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

12. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea kuweka mikakati mbalimbali katika kufanikisha majukumu yake. Miongoni mwa mikakati hiyo ni:-

i. Kuendelea kuhamasisha jamii juu ya mpango wa Serikali katika kulinda, kuhifadhi na kupanda miti ili kutimiza malengo ya kuirithisha Zanzibar ya kijani. Lengo ni kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi sambamba na kuihamasisha jamii juu ya matumizi mbadala ya nishati safi na salama.

ii. Kuendelea kuifanyia mapitio miongozo ya utendaji kazi ya Afisi yetu ikiwemo Sera ya Mazingira ya mwaka 2013, Mpango mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kufanya mapitio ya Sera ya UKIMWI Zanzibar ya mwaka 2006.

iii. Kuendelea kuwapatia vifaa saidizi watu wenye ulemavu sambamba na kuwajengea uwezo juu ya shughuli mbalimbali za kujikimu kiuchumi ili kuwa wajasiriamali.

iv. Kuendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kubadili tabia kwa kuachana na tabia hatarishi

zinazopelekea kuambukizwa kwa VVU, kuacha kujiingiza katika makundi yanayochochea matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kuepuka vitendo vya udhalilishaji kwa jamii juu ya watu wenye ulemavu kwa kuzingatia miongozo na sheria za nchi.

v. Kuendelea na maandalizi ya uandaaji wa dhana za miradi kwa ajili ya kuziwasilisha kwa wadau wa maendeleo ili kufanikisha matarajio ya Serikali na wananchi wake.

vi. Kuimarisha utendaji kazi kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wakiwemo washirika wa maendeleo ili kutimiza malengo tuliyojiwekea.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE 2020-2024.**

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miaka minne, 2020/2024 Afisi imepata mafanikio yafuatayo:-

a) Afisi imefanya tathmini 703 za kimazingira zikiwemo tathmini 318 za Athari za Kimazingira (Environmental Impact Assessment), Ripoti 184 za Ukaguzi wa kimazingira (Environmental Audit) na Ripoti 201 za kimazingira (Environmental Report). Aidha, Afisi imefanya ufuatiliaji wa kimazingira wa miradi 679 ya kiuchumi na kimaendeleo ambapo miongozo ya kimazingira imetolewa kwa miradi hiyo;

b) Afisi imefanya ufuatiliaji wa kimazingira katika maeneo 448 Unguja na Pemba, (302 Unguja na 146 Pemba). Maeneo hayo yamejumuisha mashimo ya mchanga, kifusi, mawe, kokoto, maeneo yenye matatizo ya utupaji ovyo wa taka na maji machafu, viwanda vya matofali na vituo vya kuchakata taka ambapo miongozo ya kimazingira imetolewa kwa maeneo hayo, kutatua changamoto pamoja na kuimarisha uhifadhi wa mazingira katika maeneo hayo;

c) Afisi imepunguza athari za matumizi ya mifuko ya plastiki kwa jamii na mazingira kwa kufanya operesheni 288 za kusimamia upigaji marufuku mifuko hiyo kwa Unguja na Pemba. Jumla ya tani 36 za mifuko zimekamatwa na watu 713 wamefikishwa mahakamani na kutozwa faini ya shilingi 70,810,000;

d) Afisi imepunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji holela wa mchanga na maliasili nyengine zisizorejesheka ambapo, jumla ya operesheni 179 za kusimamia maliasili hizo Unguja na Pemba zimefanyika. Katika operesheni hizo, jumla ya gari 55 aina ya canter, gari tano (5) za Ng'ombe, Misumeno ya moto saba (7) pamoja na Grenda za kupasulia mbao mbili (2) zimekamatwa na kutozwa faini ya Shilingi 28,080,000;

e) Afisi imefanya utafiti wa kina wa maeneo yanayodidimia Zanzibar ikiwemo Jang'ombe na Mwanakwerewe ili kujua sababu za kutokea hali hiyo. Utafiti huo ulibaini kuwa miongoni mwa sababu zinazopelekea kutokea hali hiyo ni watu kujenga kwenye maeneo ambayo kiasili ni maeneo yanayopokea maji mengi ya mvua;

f) Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) imefanya uchunguzi wa jiosayansi kuhusu kutomoka kwa mashimo na kudidimia kwa maeneo mbalimbali katika kisiwa cha Unguja. Uchunguzi huo umefanyika katika maeneo ya Mshelishelini, Uwanja wa Taifa - Jang'ombe, Saraevo, Ziwamaboga, na Bumbwini Misufini. Uchunguzi katika maeneo hayo umebaini kulika kwa maeneo hayo na kupelekea kuwepo kwa mashimo au mapango yaliyojaa maji na tope na kushindwa kuhimili majengo yenye uzito mkubwa;

g) Afisi imeandaa na kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani wenye lengo la kuhamasisha na kuwawezesha wananchi wote wa Zanzibar na wadau kuelewa umuhimu wa misitu, kuhifadhi miti iliyopo, kupanda na kuikuza miti ili kuimarisha mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadae ambapo uzinduzi rasmi umefanyika mwezi Agosti 2024. Kupitia programu hii jumla ya miti 60,894 ya aina mbalimbali imepandwa

ikiwemo miti 150 ya matunda, misitu na viungo katika eneo la maonesho ya biashara Nyamanzi na miti 6,700 ya matunda, miti ya misitu na viungo katika Shehia ya Matemwe kijini kwa Unguja na kwa upande wa Pemba, Serikali imepanda jumla ya mikoko 7,000 katika eneo la Gando kwa kushirikiana na CFP pamoja na jamii, mikoko 6,000 katika eneo la Muambe kwa kushirikiana na jumuiya ya GPEC, mikoko 40,000 katika eneo la Tumbe Mashariki kwa kushirikiana na KOICA, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na Jamii. Kwa upande wa Unguja Serikali imepanda mikoko 1,000 katika eneo la Uzi kwa kushirikiana na Jumuiya ya UPEPG. Aidha, Serikali imepanda miti 44 ya matunda katika majengo ya Taasisi za serikali zilizopo Gombani na katika Hospitali ya Wilaya ya Micheweni. Serikali imetoa jumla ya majiko ya gesi 1,086 kwa kushirikiana na kampuni ya ORYX Energies na kugaiwa kwa wananchi wa wilaya zote za Pemba kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati salama ya kupikia na kuweza kupunguza matumizi ya nishati ya kuni;

h) Afisi imeandaa Mpango wa Jamii wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari (Local Marine Spatial Plan) katika eneo la Zoni namba tatu ya Hifadhi ya Mkondo wa Pemba (PECCA) ambalo linajumuisha Shehia 11 zikiwemo Ndagoni, Wesha, Makombeni, Wambaa, Tibirinzi, Mizingani, Shungi, Chonga, Kilindi,

Mgelema na Mbuyuni kwa lengo la kuimarisha hifadhi hiyo; na

i) Afisi imejenga ukuta wenye urefu wa mita 500 katika maeneo ya Msuka, Wilaya ya Micheweni, Ukuta wa mita 50 katika eneo la Likoni kuelekea Kojani Wilaya ya Wete na Tuta la mita 400 limejengwa katika eneo la Tovuni Wilaya ya Wete Pemba, ambapo jumla ya wakulima 271 (wanaume 100 na wanawake 171) wamefanikiwa kurudi kwenye shughuli zao za kilimo za kuweza kujikimu kimaisha na kuyahami maeneo hayo.

j) Afisi imeandaa maandiko ya miradi mbali mbali na imeimarisha mashirikiano na Washirika wa Maendeleo katika kutekeleza Miradi na Programu mbalimbali za Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi wakiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Mfuko wa Kimazingira wa Kimataifa (Global Environmental Facility – GEF) kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazinigira – UNEP, Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Taasisi isio ya Serikali ya CAN Tanzania, Kamisheni ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Commission IOC) na Benki ya Dunia kupitia miradi ifuatayo:-

- Mradi wa kuimarisha jamii kwa kuzingatia ikolojia na shughuli za kujipatia kipato kwa

wavuvi wadogo wadogo na usimamizi wa eneo la Hifadhi la Mkondo wa PECCA - Pemba

- Mradi wa kuimarisha mfumo wa maji machafu katika eneo la Msingini, Chakechake, Pemba
- Mradi wa kuimairisha ushirikiano wa pamoja wa kujenga uhimilivu wa mifumo ya ikolojia ya baharini na pwani na jamii za wavuvi katika eneo la kusini -mashiriki wa kisiwa cha Pemba
- Mradi wa Kujenga uwezo wa utayari wa nchi katika kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa kuwa na mipango madhubuti kwenye Sera, Mikakati pamoja na mipango.
- Mradi wa Kuimarisha uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za Pwani ya Zanzibar.
- Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mfumo wa Ikilojia Vijijini (EBBAR), Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja.
- Utafiti wa kuangalia mwenendo wa ushiriki wa taasisi za Serikali pamoja na jamii kwa kuzingatia masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi katika mipango yao.
- Tathmini ya athari ya Mabadiliko ya Tabianchi katika Kisiwa cha Pemba kupitia NAP -Global Network

k) Afisi imewezesha upatikanaji wa boti sita na vifaa vya uvuvi vikiwemo GPS, mashine, nyavu na kifaa cha kuangazia samaki kwa Shehia tatu za Matemwe (Mbuyutende, Jugakuu na Kijini) zinazotekeleza mradi wa EBBAR.

l) Afisi imeanzisha na kusimamia mfumo wa kuhifadhia taarifa za Watu wenye Ulemavu – Zanzibar ambapo jumla ya Watu wenye Ulemavu 8,615 (wanawake 4,070 na wanaume 4,545) wamesajiliwa kupitia mfumo huo;

m) Afisi imewaendeleza kielimu vijana wenye Ulemavu 98 katika vyuo vya mafunzo ya amali ambapo wanaumme 62 na wanawake 36;

n) Afisi imeongeza upatikanaji wa vifaa saidizi kwa Watu wenye Ulemavu ambapo jumla ya vifaa visaidizi 1,381 vyenye thamani ya Shilingi 349,130,000 vimetolewa Unguja na Pemba, (Unguja visaidizi 720 vimetolewa (wanawake 434 na wanaume 286) na kwa Pemba visaidizi 661 (wanawake 411 na wanaume 250);

o) Afisi imezipatia ruzuku Jumuiya 12 za Watu wenye Ulemavu zenye thamani ya TZS. 30,000,000 Unguja na Pemba pamoja na mikopo kwa Watu wenye Ulemavu yenye thamani ya TZS. 30,000,000 (Unguja TZS.22,000,000 na Pemba TZS. 8,000,000) kwa ajili ya kujishughulisha na kazi za uchumi na maendeleo. Fedha hizo zimetolewa

kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) kupitia Programu ya 4:4:2 kwa vikundi saba (7) ikiwemo Juhudi mbele Kizimkazi, Tushirikiane Tumbatu, Nia safi Masingini na Walemavu kwanza Kitope kwa Unguja na Kikundi cha Nguvu moja, Tujitegemee na Molatubariki vya Pemba.

p) Watuhumiwa 1,220 (wanaume 1,169 na wanawake 51) wamekamatwa wakihusishwa na kesi za dawa za kulevya zikiwemo bangi kesi 757, heroin kesi 463, mirungi kesi 19, kokeni kesi 9, codeine kesi 3 valium kesi 5, mandrax kesi 1, morphine kesi 2, na methamphetamine kesi 1. Katika kesi hizo, kesi 1,198 zilifunguliwa ambapo kesi 755 zimefikishwa Mahakamani kwa hatua za kisheria;

q) Afisi imeteketeza vielelezo vya dawa za kulevya vyenye uzito wa Kilogramu 1,619.86 (1,448.9 - Unguja na 170.9 - Pemba)

r) Afisi imekamilisha ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia kwa waraibu wa dawa za kulevya kilichopo Kidimni chenye thamani ya Shilingi 5,151,490,133. Vile vile, OMKR imefanya ukarabati mkubwa wa Nyumba ya Mapumziko ya Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais ilioko Micheweni Pemba kwa thamani ya Shilingi 497,470,915.

s) Kuanzishwa kwa mawasiliano ya moja kwa moja na wanajamii ambapo nambari ya simu ya bure

(0774 333 300) imetolewa kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya. Kupitia simu hiyo jumla ya taarifa 415 ziliripotiwa na kufanyiwa kazi.

t) Kuteuliwa kwa Majaji na Mahakimu maalumu kwa ajili ya kusikiliza kesi za dawa za kulevya, ambapo kesi 755 zilizofikishwa Mahkamani, kesi 179 zimepata hatia, kesi 273 zimeachiwa huru na kesi 171 zinaendelea; Mahkamani. Aidha, mali zenye thamani ya shilingi Bilioni (15,334,000,000 zinazohusiana na dawa za kulevya zimekamatwa na kutaifishwa zikiwemo gari 8, boti 3, honda 1, nyumba 12 na viwanja 10.

u) Kuanzishwa kwa Kituo cha Transnational Organised Crime Task Force kilichojumuisha watendaji kutoka TRA, DPP, ZDCEA, Chuo cha Mafunzo, KMKM, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Zanzibar chini ya ufadhili wa Serikali ya Uengereza kupitia Shirika la UNDP;

v) Kutungwa na kufanyiwa marekebisho ya sheria Nam.8 ya mwaka 2021, Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kuongeza vifungu 2 kurekebisha vifungu 6 na kufuta vifungu 4 iliyopelekea kuanzishwa na kuipa nguvu Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar.

w) Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) pamoja na wadau mbali mbali wa ndani na wa kikanda imefanikiwa kuwakamata jumla ya wahalifu 6 wa kimataifa wa dawa za kulevya (wanaume 4 na wanawake 2).

x) Utafiti wa tathmini ya maambukizi ya UKIMWI kitaifa uliofanywa mwaka 2020/2023 umeonesha kwamba Zanzibar imepunguza maambukizi mapya ya VVU kutoka watu 519 mwaka 2020 hadi watu 362 mwaka 2023 na idadi ya watoto wanaozaliwa na VVU imepungua kutoka asilimia 3.6 mwaka 2020 hadi asilimia 1.5 mwaka 2023.

y) Idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI vimepungua kutoka vifo 274 mwaka 2020 hadi vifo 190 mwaka 2024.

z) Afisi imeimarisha utoaji wa huduma za masafa kwa makundi maalum ili kuzuia maambukizo mapya na kuwapatia huduma za VVU ambapo jumla ya watu 62,538 wa makundi maalumu wamefikiwa na 41,752 walikubali kupima VVU ambapo 145 waligundulika na maambukizo ya VVU.

aa) Afisi imekamilisha uandaaji wa miongozo mbali mbali ili kukabiliana na maradhi ya UKIMWI ikiwemo:-

- Mkakati wa IV wa Kitaifa wa kupambana na UKIMWI kwa kipindi cha mwaka 2022-2027 unaozihusisha sekta zote za Serikali na zisizo za Serikali;
- Mkakati wa mawasiliano na utetezi wa VVU na UKIMWI kwa vijana kwa kipindi cha 2023-2027;
- Muongozo wa uzingatiaji wa masuala ya UKIMWI katika miradi ya maendeleo

bb) Kwa kushirikiana na mfumo wa SNR Mwinyi, Afisi, imeimarisha utoaji wa huduma na utatuzi wa kero za jamii ambapo jumla ya Kesi 161 zimetatuliwa na kesi 12 zinaendelea kupatiwa ufumbuzi kati ya malalamiko 173 yaliyowasilishwa.

cc) Afisi imetoa jumla ya TZS. 27,870,000 kwa jamii ikiwa ni usaidizi wa utatuzi wa changamoto kwa huduma mbali mbali za kijamii ikiwemo vifaa vya ujenzi, Computer, Printer na vifaa vya michezo.

dd) Afisi imeandaa na kuchapisha Mpango Mkakati wa utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2021 – 2026;

ee) Afisi imeratibu na kuandaa sera, sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ikiwemo sera ya dawa za kulevya ya mwaka 2023, sheria ya kudhibiti na

kupambana na dawa za kulevya namba 8 ya mwaka 2021, sheria ya Watu wenye ulemavu namba 8, 2022, kanuni ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya yam waka 2023 na muongozo wa ufuatiliaji ya miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu.

## UKUZAJI WA HUDUMA KWA JAMII KATIKA UJENZI WA UCHUMI IMARA NA SALAMA, SHIRIKISHI, ENDELEVU NA HIMILIVU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

14. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeendelea kusimamia masuala mtambuka yakiwemo usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kusimamia upatikanaji wa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu, mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya, kuimarisha upatikanaji wa kinga na tiba ili kumaliza maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI ifikapo 2030.

15. **Mheshimiwa Spika,** juhudi za kuendelea kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi wa mazingira zimeongezeka ambapo jumla ya maeneo mawili (2) yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi yemechukuliwa hatua stahiki kwa kujengewa kuta za kuzuia maji ya bahari yasiingie katika maeneo ya makaazi na kilimo katika eneo la SIPWESE mita 312 (eneo A mita 195 na eneo B mita 117) na Kisiwa Panza mita 70 kwa thamani ya TZS 298,508,950 kwa mwaka

2024/2025 ikilinganishwa na mwaka 2023/2024 ambapo ni eneo moja tu la mita 400 Tovuni kwa Thamani ya TZS 234,702,262.

16. **Mheshimiwa Spika,** jitihada mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa katika kuimarisha usimamizi wa mazingira ikiwemo kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya kilogramu 481 zimekamatwa ikilinganishwa na kilogramu 400 zilizokamatwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Haya ni mafaniikio makubwa yaliyopatikana katika udhibiti wa mifuko ya plastiki ambapo kwa kipindi cha miaka minne wastani wa tani tisa (9) zilikamatwa kwa mwaka. Vile vile, kuongezeka kwa doria za usimamizi wa misitu na maliasili zisizorejesheka ambapo jumla ya doria 157 kwa mwaka 2023/2024 na doria 185 kwa mwaka 2024/2025. Uhifadhi wa mazingira kwa ujenzi wa msingi wa kukusanya maji machafu wenye urefu wa mita 100 pamoja na kuunganisha kaya 147 katika ukusanyaji wa maji taka umefanyika katika eneo la Msingini Kusini Pemba yenye thamani ya shilingi 133,221,175 pamoja na upandaji wa miti 40,536 ikiwemo miti ya misitu, matunda katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba kupitia Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani.

17. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeimarisha upatikanaji wa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu, ambapo kwa mujibu wa

Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022 imeonesha ongezeko la Watu wenye Ulemavu kutoka asilimia 5.8 kwa mwaka 2012 hadi 11.4 kwa mwaka 2022 kwa wastani wa Watu wenye Ulemavu 195,772. Aidha,katika kuhakikisha kutoa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu, jumla ya vifaa saidizi 852 vyenye thamani ya shilingi Milioni 118,400,000 vimetolewa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ikilinganishwa na vifaa saidizi vya kisasa na vyenye ubora 425 vyenye thamani ya shilingi Milioni 325,500,000 kwa mwaka 2024/2025 na utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa Watu wenye Ulemavu kutoka watu 96 kwa mwaka 2023/2024 hadi watu 71 kwa mwaka 2024/2025. Vile vile, utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Watu wenye Ulemavu umeongezeka kutoka vikundi saba (7) kwa mikopo ya shilingi 30,200,000 kwa wanufaika 76 (wanawake 34 na wanaume 42) kwa mwaka 2023/2024 hadi vikundi 11 kwa mikopo ya shilingi Milioni 43,200,000 kwa wanufaika 144 (wanawake 83 na wanaume 61) kwa mwaka 2024/2025. Baraza la Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limetoa unafuu wa masharti ya mikopo ya Watu wenye Ulemavu kupitia programu ya 4:4:2 ambapo inatoa fursa kwa mjasiriamali mmoja mmoja mwenye Ulemavu kuweza kupata mikopo hiyo. Mabadiliko haya yatatoa fursa ya mikopo kwa Watu wengi zaidi wenye Ulemavu.

18. **Mheshimiwa Spika,** mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya yameimarika ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kilogramu 957 za dawa za kulevya zilikamatwa pamoja na kutaifisha mali zenye thamani ya TZS 15,334,000,000 ikilinganishwa na kilogramu 1449 za dawa zilizokamatwa na mali zilizotaifishwa zenye thamani ya TZS 976,052,016 kwa mwaka 2024/2025. Aidha, mafanikio haya yametokana na mabadiliko ya sheria iliyopelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana dhidi ya dawa za Kulevya iliyopewa uwezo wa kukamata, kushtaki pamoja na kutaifisha mali zitokanazo na biashara haramu za dawa za kulevya. Vilevile, Mamlaka imekuwa na uwezo wa kuimarisha mashirikiano na Taasisi na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa ya Kupambana na dawa za kulevya.

19. **Mheshimiwa Spika,** katika mapambano ya kutokomeza maambukizi ya VVU na UKIMWI Afisi imefanya utafiti wa hali ya UKIMWI kwa kipindi cha miaka mitano 2022/2023 na kubaini kwamba idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeendelea kuwa chini ya asilimia 1. Aidha, utafiti umeonesha kwamba asilimia 0.4 ya wakaazi wa Zanzibar wanaishi na virusi vya UKIMWI ikiwa ni sawa na watu 10,580 (Unguja asilimia 0.5 na Pemba asilimia 0.3). Pia, utafiti huo umeonesha kwamba mkoa wa kusini Unguja una kiwango kikubwa cha watu wanoishi na virusi vya UKIMWI (asilimia 0.8) ukifuatiwa na Mkoa wa

Kaskazini Unguja wenye asilimia 0.7, Mkoa wa Kusini Pemba ni asilimia 0.5, Mkoa wa Mjini Magharibi ni asilimia 0.4 na Mkoa wa Kaskazini Pemba ndio wenye kiwango cha chini cha watu wenye kuishi na virusi vya UKIMWI kwa asilimia 0.2. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa Mkakati wa kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030, Mkakati wa Mawasiliano na Utetezi unaochochea mabadiliko ya tabia kwa vijana pamoja na kuimarika kwa utoaji wa huduma masafa kwa makundi maalum katika kuzuwia maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI.

## C. UTEKELEZAJI WA MALENGO YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA WA 2024/2025.

20. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilijiwekea malengo yafuatayo: -

i. Kuendeleza utekelezaji wa Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani;

ii. Kutayarisha mpango wa kitaifa wa mazingira;

iii. Kufanya utafiti katika eneo la dawa za kulevya pamoja na Watu wenye Ulemavu;

iv. Kuimarisha programu za UKIMWI kwa vijana na makundi maalumu;

v. Kujenga kituo cha tiba na marekebisho ya tabia Pemba; na

vi. Kuendelea kuimarisha ushirikiano baina ya SMT na SMZ.

21. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilitekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu saba (7) ambazo ni:-

i. Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi;

ii. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;

iv. Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya;

v. Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI;

vi. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; na

vii. Programu ya Usimamizi wa Mazingira

22. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliendelea kusimamia miradi sita (6) ya maendeleo kama ifuatavyo:-

i. Mradi wa kuirithisha Zanzibar ya kijani unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

ii. Mradi wa kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za pwani ya Zanzibar unaofadhiliwa na mfuko wa Mazingira (Adaptation Fund;)

iii. Mradi wa uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mfumo wa ikolojia vijijini (EBBAR) unaofadhiliwa na UNEP;

iv. Mradi wa usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika;

v. Mradi wa ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

vi. Mradi wa ujenzi wa nyumba ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

23. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeendeleza mashirikiano na Taasisi mbali mbali zikiwemo UNEP, UNDP, IOC, Taasisi ya Uongozi Tanzania na Asasi za kiraia (NGO) ya CAN-TZ katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazingira na kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kama ifuatavyo:-

i. Mradi wa kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa jamii ya pwani katika maeneo ya Bumbwini Mafufuni-Unguja, Kiongwe kidogo na Tovuni kwa upande wa Pemba

ii. Mradi wa uimarishaji na utanuzi wa mtaro wa maji machafu katika eneo la Msingini-Pemba

iii. Mradi wa kuimarisha jamii kwa kuzingatia ikolojia na shughuli za kujipatia kipato kwa wavuvi wadogo wadogo na usimamizi wa eneo la hifadhi la mkondo wa PECCA- Pemba

iv. Tathmini ya kuangalia athari ya mabadiliko ya tabianchi katika kisiwa cha Pemba

## MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### Mapato

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 619,947,000 kupitia vyanzo vya mapato ambavyo ni ada ya uhifadhi wa mazingira na ada ya ukaguzi wa mazingira. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya Shilingi Milioni 470,500,000 zilipangwa kukusanywa ambapo jumla ya Shilingi Milioni 305,195,000 sawa na asilimia 65 zimekusanywa. **Kiambatanisho nam. 6 kinahusika.**

**Matumizi**

25. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imetekeleza majukumu yake kupitia mfumo unaotumia Programu (PBB) kupitia mafungu manne (4) ya bajeti ambayo ni fungu B01 (Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais), fungu B04 (Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira), C04 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya) na C05 (Tume ya UKIMWI).

26. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Afisi iliidhinishiwa matumizi ya shilingi 19,057,370,840 ambapo Matumizi mengineyo shilingi 12,460,286,000, Miradi ya Maendeleo shilingi 6,597,084,840 na Ruzuku ya TZS. 280,000,000. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilipangiwa matumizi ya Shilingi Bilioni 9,816,631,250 katika utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi Bilioni 4,712,236,492 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi Bilioni 4,888,144,758 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na Ruzuku ni Shilingi Milioni 216,250,000. Hadi kufikia mwezi Machi 2025, jumla ya Shillingi Bilioni 6,787,134,220 sawa na asilimia 69 zilipatikana kwa kazi za kawaida ambapo Shillingi Bilioni 4,320,746,170 sawa na asilimia 92 ni kwa mishahara na Shilingi Bilioni 2,395,720,050 sawa na asilimia 49 ni kwa matumizi mengineyo na Shilingi Milioni 70,668,000 ni kwa ajili ya matumizi ya Ruzuku sawa na asilimia 33. **Kiambatanisho nam. 7A kinahusika.**

27. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kazi za maendeleo, kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 jumla ya Shilingi Bilioni 6,597,084,840 ziliidhinishwa ambapo shilingi 6,050,000,000 kutoka SMZ na 547,084,840 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilipangiwa kutumia Shilingi Bilioni 4,089,584,840 ambapo shilingi Bilioni 3,542,500,000 kutoka SMZ na shilingi Milioni 547,084,840 kutoka kwa Washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya shilingi 691,173,316 (SMZ 478,942,196 na 212,231,120 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia **17** zilipatikana. **Kiambatanisho nam. 13 kinahusika.**

## D. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

28. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imepata mafanikio makubwa katika kuleta maendeleo ya kisekta kama ifuatavyo:-

    i. Afisi imejenga ukuta wenye urefu wa mita 70 katika eneo la kisiwa panza – Pemba jambo ambalo limesaidia katika jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuzuia maji ya chumvi kuingia katika maeneo ya kilimo na makaazi ya wananchi;

ii. Afisi imeziunganisha nyumba (kaya) 147 katika mfumo wa kudhibiti maji machafu katika eneo la Msingini Chakechake Pemba, jambo ambalo limesaidia kudhibiti mripuko wa maradhi yanayo sababishwa na kuenea kwa maji taka katika jamii;

iii. Afisi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inatekeleza Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani ambapo imeimarisha suala la upandaji wa miti, jumla miche 20,736 imetolewa kwa wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Vikosi maalum vya SMZ na vikundi vya jamii na imepandwa katika maeneo mbalimbali wanayoyasimamia;

iv. Kuhamasika kwa jamii katika uhifadhi wa mazingira ambapo jumla ya vikundi 45, vinavyojumuisha taasisi na mashirika yameomba kupatiwa miche ya aina mbali mballi, ongezeko la uzalishaji wa miche katika vitalu vya watu binafsi na Serikali na upandaji wa miti katika maeneo mbali mbali;

v. Afisi imewapatia wananchi mitungi ya gesi 1,129 kwa ajili ya kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia kwa wananchi mbali mbali Unguja na Pemba;

vi. Afisi imefanya tathmini ya sekta zinazoathirika na mabadiliko ya tabia nchi (sectorial vulnerability assessment 2024/2025) zikijumuishaa sekta ya utalii, afya, kilimo, misitu, mifugo, mawasiliano, ardhi, nishati, uvuvi na uchumi wa buluu kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo wa Utayari wa Nchi Kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kuandaa Mpango wa Taifa wa Kujumisha athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mipango ya Taifa (NAP);

vii. Afisi imeziwezesha shehia tatu za Matemwe kwa kuzipatia njia mbadala za kujiongezea kipato ikiwemo kuanzishwa kwa kituo cha ushoni na upakasaji, kituo cha utengezaji wa sabuni pamoja na kujenga mabanda ya kufugia kuku na mbuzi na kupatiwa mizinga 120 kwa ajili ya ufugaji wa nyuki kupitia mradi wa EBBAR ambapo jumla ya watu 71 wamenufaika;

viii. Afisi imewajengea uwezo Watu wenye Ulemavu 71 (wanaume 33 na wanawake 38) kwa kuwalipia gharama za masomo jumla ya shilingi 53,773,000 katika ngazi za cheti na astashahada;

ix. Afisi imeendelea na uwekaji wa taarifa katika mfumo wa Watu wenye Ulemavu ambapo hadi sasa jumla ya Watu wenye Ulemavu 16,661 wamesajiliwa;

x. Afisi imetoa vifaa saidizi vya kisasa na vyenye ubora 425 kwa Watu wenye Ulemavu vyenye thamani ya shilingi 325,500,000 Unguja na Pemba;

xi. Utafiti wa hali halisi ya Watu wenye Ulemavu nchini Tanzania umefanyika ambapo masuala ya ajira, huduma za Kijamii, Miundombinu na Udhalilishaji yamezingatiwa. Aidha utafiti huo umeonesha uimarishaji wa utoaji wa huduma za kijamii na miundombinu rafiki kwa watu wenye Ulemavu.

xii. Afisi imekamilisha ujenzi wa kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni ambapo jumla ya waraibu 132 wamepokelewa. Aidha, katika mwaka 2024/2025 waraibu 25 wamefanikiwa kuachana na matumizi ya dawa za kulevya ambapo wamepatiwa vifaa mbali mbali vya ujasiriamali vikiwemo charahani kimoja, zana tatu za ufundi na Ng'ombe mmoja vilivyogharimu shilingi 4,000,000, waraibu 51 wamekatisha huduma, waraibu 41 wanaendelea na huduma na waraibu 10 wamejiunga na miradi ya ujasiriamali.

xiii. Afisi imekamata na kutaifisha mali zinazohusishwa na biashara ya dawa za kulevya zenye thamani ya shilingi Milioni 976,052,016 kutoka kwa wahalifu wa dawa za kulevya.

xiv. Afisi imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya pamoja na Sheria Nambari 8 ya mwaka 2021 katika maeneo mbali mbali ikiwemo taasisi za elimu, masheha, wananchi, vikosi vya Ulinzi na Usalama na maeneo ya kazi kwa Unguja na Pemba ambapo jumla ya wanafunzi 7,343 (wanaume 3228 na wanawake 4,115) na walimu 71 walipatiwa elimu kutoka skuli mbali mbali. Aidha, shehia za Bumbwini, Langoni, Marumbi, Mpapa, Muyuni, Mahonda, Gana, Donge na Amani kwa Unguja na Shehia za Wesha, Gando, Mchanga Mrima, Mbuzini, Vitongoji na Ngwachani kwa Pemba zilifikiwa na jumla ya wananchi 1139 (wanaume 625, wanawake 514) walipatiwa elimu. Pia elimu ilitolewa kupitia vyombo vya habari na vipindi 6 vilirikodiwa na kurushwa hewani kupitia Zanzibar Cable Television, Bahari FM Redio na ZBC TV.

xv. Kuimarisha mashirikiano kwa kusaini hati za makubaliano baina ya Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na Madawa ya Kulevya SMZ na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (ZDCEA na DCEA) pamoja na Mamlaka ya usimamizi wa mazingira (ZEMA) na Mamlaka ya usafiri baharini. (ZMA). Lengo ni kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na kubalishana mbinu zikazoleta ufanisi katika utoaji wa huduma kwa Wananchi.

xvi. Afisi imekamilisha mapitio ya Mkakati wa Kitaifa wa Kondomu (2024-2029) ili kuhakikisha unaenda sambamba na Mkakati wa Nne wa Taifa wa UKIMWI

xvii. Afisi imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa VVU na UKIMWI wa vyuo vya mafunzo na mpango endelevu wa muitiko wa taifa wa UKIMWI unaolenga kuongeza fedha za ndani kwa mapambano dhidi ya UKIMWI

xviii. Mapambano dhidi ya kutokomeza UKIMWI yameendelea ambapo jumla ya watu 4,549 wamepatiwa elimu kupitia mitandao ya kijamii, jumla ya vipeperushi 317, majarida 32, vifaa 101 vya JIPIME na kondomu za kiume 2,160 viligaiwa kwa watu wenye uhitaji katika maonesho mbali mbali ya kitaifa.

xix. Afisi imetoa elimu na huduma za VVU kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Unguja na Pemba kupitia mijadala na huduma za masafa. Vyuo vilivyoshiriki ni Chuo Kikuu cha Taifa Tunguu, Karume Institute of Science and Technology (KIST), Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Chuo cha Utawala wa Umma (IPA), Zanzibar Business School (ZBS), Chuo cha Afya Mbweni na Chuo cha Kiislamu kwa upande wa Unguja na Chuo cha Mwalimu Nyerere kwa upande wa Pemba.

xx. Kanuni ya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa ya mwaka 2024 na kanuni ya biashara ya hewa ya kaboni ya mwaka 2020/2025 zimekamilika na kutangazwa katika gazeti rasmi la Serikali nambari CXXXIII No. 7270 la tarehe 23 Agosti, 2024 na nambari Vol.CXXXIV No. 7319 la tarehe 14 Machi, 2025.

xxi. Ulinzi na usalama wa ofisi umeimarishwa kwa kuwekwa mfumo wa CCTV Camera katika jengo zima la ofisi uliogharimu shilingi 30,000,000.

xxii. Wizara imeendelea na utoaji wa stahiki za wafanya kazi zikiwemo likizo kwa wafanyakazi 73, malipo baada ya saa za kazi za ziada 28, mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 26 na muda mfupi wafanyakazi 11 na fedha za ubani kwa wafanyakazi watano. Vile vile, Afisi kwa kushirikiana na Afisi ya Rais, Katiba Sheria na Utawala Bora imetenga posho maalumu kwa ajili ya kupatiwa Maafisa wa operesheni wa dawa za kulevya.

## CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

## CHANGAMOTO

29. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inakabiiliwa na changamoto zifuatazo :-

i. Ufinyu wa bajeti ambao hauendani na mahitaji ya utekelezaji wa majukumu ya Afisi ambao pia unapelekea upungufu wa vifaa na vyombo vya usafiri;

ii. Jamii kuwa na muhali katika kutoa taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya na Unyanyapaa kwa watu wenye Ulemavu;

iii. Jamii kuchukulia maambukizi ya VVU na UKIMWI kuwa sio tatizo tena kunakopelekea kufanyika kwa vitendo hatarishi vya kupata maambukizi ya VVU;

iv. Washirika wa maendeleo kupunguza nguvu za usaidizi katika suala la VVU na UKIMWI;

v. Kuongezeka kwa mmong'onyoko wa maeneo ya fukwe na maeneo 147 yanayoingia maji ya chumvi Unguja na Pemba ambayo yanapelekea mahitaji makubwa ya rasilimali fedha katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

vi. Kuendelea kwa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya misitu, bahari na maliasili zisizorejesheka

## HATUA ZA KUTATUA CHANGAMOTO

30. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Rais imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo zikiwemo:-

i. Afisi imeshawasilisha makisio ya fedha na mahitaji ya gari katika Afisi ya Rais, Fedha na Mipango ambapo hadi sasa imepokea gari saba (7) kwa matumizi ya Afisi na Taasisi zake na

imepata fedha na kununua vifaa mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utekelezaji. Aidha, jumla ya gari Nne (4) zinatarajiwa kuwasilishwa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 na kuongezewa bajeti ya TZS.110,000,000 kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 kwa ajili ya ununuzi wa gari kwa Idara ya Mazingira;

ii. Kuendelea kukuza uelewa kwa jamii juu ya athari za matumizi ya Dawa za Kulevya na kuondoa muhali, kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI, unyanyapaa wa Watu wenye Ulemavu kupitia majukwaa, makundi tofauti na vyombo vya habari. Aidha, Baraza la Watu wenye ulemavu linaedelea na kuimarisha mahusiano mema na Taasisi mbalimbali ikiwemo Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi (ZEEA) yaliyopelekea kupunguza masharti ya Mikopo ya 4:4:2 kwa Watu wenye Ulemavu kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa mikopo nafuu;

iii. Katika Kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imepata jumla ya TZS 4,500,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi na usimamizi wa Mazingira katika bajeti ya mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka 2024/2025 ambapo jumla ya TZS. 500,000,000 zilizoidhinishwa. Vilevile, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa

kushirikiana na Afisi ya Makamo wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa andiko la Mradi wa Kuimarisha mifumo ya Kitaifa na kuziwezesha Serikali za Mitaa kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi, ambao utatekelezwa katika Wilaya 56 za Tanzania ikiwemo Wilaya 11 za Zanzibar kwa kipindi cha miaka 5. Mradi unafadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo jumla ya shilingi 317,680,000,000 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo utakaoanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026.

iv. Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Afya inachukua juhudi mbali mbali katika kuhakikisha kwamba huduma kwa waathirika wa UKIMWI wanapata huduma stahiki ikiwemo upatikanaji wa dawa za ARV, mipira ya kondomu, upimaji wa hiyari na elimu juu ya maradhi nyemelezi katika kustawisha afya zao. Aidha, baada ya kukamilika kwa kipindi cha mpito cha miezi mitatu ya tathmini ya miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani imethibitisha kuendelea na utoaji wa misaada kwa miradi ya VVU na UKIMWI. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya tathmini ya uwepo wa dawa za UKIMWI na kubainika kwamba kwa kipindi cha miaka miwili hakutokuwa na shida ya dawa kutokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuongeza bajeti ya ununuzi wa dawa kupitia Wizara ya Afya na kuendelea kupokea dawa za msaada kutoka Shirika la GEF.

v. Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Maji Nishati na Madini, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara maalumu za SMZ pamoja na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imeunda kikosi kazi cha doria kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira. Vile vile Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imezindua programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani kwa lengo la kuendeleza na kuirudisha misitu pamoja na kuweka udhibiti wa utoaji wa vibali na utaratibu mzuri wa uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

## E. UTEKELEZAJI WA MALENGO KUPITIA PROGRAMU ZA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA KWA RAIS KUANZIA JULAI 2024 – MACHI 2025.

31. **Mheshimiwa Spika,** Afisi inatekeleza majukumu yake kupitia Mfumo wa Bajeti unaotumia Programu (PBB) kupitia Programu Kuu saba na Programu ndogo 18 ambapo fedha za matumizi zinapitia mafungu manne ya bajeti ambayo ni fungu B01 (Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais), fungu B04 (Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira), C04 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya) na C05 (Tume ya UKIMWI) kama ifuatavyo:-

## MATUMIZI YA FUNGU B01 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS)

**32. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kupitia fungu B01 (Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais) ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 10,266,384,840 (Mshahara shilingi Bilioni 3,264700000, matumizi mengineyo shilingi Bilioni 2,674,600,000, ruzuku shilingi Milioni 280,000,000 na shilingi Bilioni 4,047,084,840 kwa miradi ya maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Afisi ilikadiriwa kutumia Shilingi 6,978,743,107 Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 2,226,611,500 ni kwa ajili ya Mishahara; Shilingi Bilioni 2,358,796,767 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Shilingi 216,250,000 ni kwa ajili ya Ruzuku; Bilioni 2,177,084,840 ni kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi Bilioni 1,630,000,000 kutoka Serikalini na shilingi Milioni 547,084,840 kutoka kwa Washirika wa maendeleo.

**33. Mheshimiwa Spika,** Kupitia fungu B01, Shilingi 2,754,344,926 ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; Shilingi 1,031,677,875 kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Watu wenye Ulemavu, shilingi 2,123,803,595 ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu Uratibu wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais na shilingi 2,472,185,219 kwa ajili ya kutekeleza Programu

Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. **Kiambatanisho namba 7A kinafafanua**

34. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, fedha zote zilizoingizwa ni Shilingi 3,472,338,654 ambayo ni sawa na asilimia 50 ya utekelezaji. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,142,166,292 ni kwa ajili ya Mishahara ambayo sawa na asilimia 96; Shilingi 779,562,266 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo sawa na asilimia 33; Shilingi 70,668,000 ziliingizwa kwa matumizi ya Ruzuku ambayo sawa na asilimia 33 na shilingi 566,133,489 (SMZ 353,902,369 na wahisani 212,231,120) kwa ajili ya kazi za maendeleo.

35. **Mheshimiwa Spika,** fedha zilizopatikana kupitia programu za fungu B01, Shilingi Milioni 847,836,053 ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; Shilingi 608,220,329 kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Watu wenye Ulemavu, shilingi 664,305, 916 kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu Uratibu wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais na shilingi 1,439,067,649 kwa ajili ya programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

### Programu Kuu PB0101: Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kuwa na mazingira endelevu pamoja na kupungua kwa athari za mabadiliko ya tabianchi

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2024/2025 iliidhinishiwa shilingi Bilioni 3,145,841,622 (Mshahara ni shilingi Milioni 349,976,782 na matumizi mengineyo shilingi Milioni 248,780,000 na shilingi Bilioni 2,547,084,840 kwa miradi ya maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ilipangiwa kiasi cha Shilingi Bilioni 2,555,009,195mpaka kufikia mwezi Machi, 2025 imepatiwa matumizi ya Shilingi Milioni 847,936,053 ambapo Matumizi ya Kawaida 28,880,893 na Mishahara 252,821,671 na maendeleo 566,133,489 (SMZ 353,902,369 na 212,231,120 kutoka kwa wahisani) sawa na asilimia 75 ya utekelezaji programu zake ndogo.

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kipindi cha Julai – Machi mwaka 2024/2025, imetekeleza yafuatayo:-

a) Afisi imeshiriki maonesho, warsha na mikutano ya ndani na nje ya nchi ikiwemo warsha ya siku tano mjini Helsinki, nchini Finland juu ya matumizi ya njia za kitaalamu na teknolojia za kisasa za ukusanyaji wa taarifa za mazingira ya bahari ili kusaidia njia bora

za kuhimili mabadiliko ya tabianchi, mkutano wa nne wa kikundi kazi cha mkakati wa utekelezaji wa Mkataba wa Basel wa nchi wanachama uliofanyika mjini Geneva, Switzerland, mkutano wa 29 wa nchi wanachama wa mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi mjini Baku, Azerbaijan, mkutano wa 16 wa nchi wanachama wa mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Bioanuai nchini Colombia.

b) Afisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi na Chuo Kikuu cha Dar – es – salaam imefanya utafiti juu ya mifumo ya Utawala wa masuala ya mabadiliko ya Tabianchi katika Mipango ya Serikali (Exploring the Role of Governnance Frameworks in Fostering Climate Change Adaptation in Zanzibar) na Utafiti huo upo katika hatua za mwisho za kukamilika.

c) Afisi imejenga ukuta wa kuzuia maji ya bahari kuingia katika mashamba ya kilimo katika eneo la Shehia ya Kisiwa Panza chini ya mkandarasi wa kampuni na KIN Investment umekamiliika.

d) Afisi kupitia Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mfumo wa Ikolojia Vijijini, inaendelea na ujenzi wa mabanda matatu ya kufugia kuku na banda moja la kufugia mbuzi, mashine tatu za kutotolea vifaranga "Incubator" na seti 60 za vifaa vya kufugia nyuki kwa Shehia tatu zinazotekeleza mradi zimenunuliwa. Aidha, mafunzo ya ushoni wa vyerehani na upakasaji kwa wanajamii 77 kutoka

vikundi vitatu vya ushoni wa vyerehani na upakasaji katika shehia zinazotekeleza mradi yamefanyika.

e) Programuu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani ilizinduliwa tarehe 17/08/2024 katika Kiwanja cha Maonesho ya Taifa cha Biashara Nyamanzi ambapo jumla ya miti 20,194 ilipandwa Unguja na Pemba. Jumla ya watu 180 kutoka Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (KMKM, Chuo cha Mafunzo, Zima Moto, JKU na KVZ) wameshiriki katika mkutano wa utekelezaji wa Programu hiyo. Aidha, jumla ya miche 14,292 ya miti ya matunda na misitu imetolewa kwa vikosi hivyo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wake. Vile vile, Warsha ya miongozo ya urejeshaji wa maliasili za bahari kwa watumiaji wa eneo namba 3 la mkondo wa PECCA ilifanyika ambapo wajasiriamali wanawake 77 walijengewa uelewa juu ya ushoni wa vyerehani na upakasaji katika shehia tatu za Matemwe (Jugakuu, Mbuyutende na Kijini).

f) Kupitia mradi wa SAPPHIRE, Afisi kwa kushirikiana na Idara ya Misitu Pemba, ilifanya utambuzi na upimaji kwa ajili ya kuanzisha hifadhi ya misitu ya jamii (COFMA) katika eneo la msitu wa mikoko wa Tibirinzi. Lengo la utambuzi na upimaji huo ni uhifadhi na utunzaji wa misitu pamoja na kuangalia uwezekano wa kuanzia biashara ya kaboni. Vilevile, Afisi imeshiriki katika kuandaa andiko la mradi wa jamii wa kujipatia kipato kwa kuanzisha uhifadhi wa misitu ya mikoko kwa ajili ya shughuli za utalii katika eneo la Tibirinzi, Pemba.

g) Afisi kupitia mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Maji Machafu, Chake chake-Pemba imeunganisha nyumba 147 katika mfumo wa maji machafu chini kampuni ya Ngenda iliyoko Pemba. Lengo ni kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuzuia kuenea kwa maji taka katika maeneo ya makaazi ya watu.

h) Afisi imeshiriki katika maonesho ya kitaifa ya Kilimo yaliyofanyika katika eneo la Maonesho ya Kilimo Dole - Wilaya ya Magharibi "A" Unguja, ambapo jumla ya wananchi 103 walitembelea banda la Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kupatiwa elimu ya Mazingira. Aidha, Afisi imeshiriki mikutano ya kupitia ripoti mbalimbali zilizoandaliwa kupitia Mradi wa Kujenga uwezo wa utayari wa nchi kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Morogoro. Vilevile, Afisi imeshiriki warsha ya Ujumuishaji wa Uhamaji na Uhamiaji wa binaadamu katika Mipango ya Taifa ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi iliyofanyika nchini Uganda pamoja na kushiriki mafunzo ya muda mfupi ya matumizi ya bioteknolojia katika kilimo yaliyofanyika nchini Marekani.

**Programu Kuu PB0102: Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu**

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kukuza upatikanaji na Ufikiwaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu

38. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2024/2025 iliidhinishiwa shilingi Bilioni 1,279,089,813 (Mishahara

Milioni 551,299,813 na matumizi mengineyo shilingi Milioni 447,790,000 na ruzuku ya shilingi Milioni 280,000,000). Programu hii Kuu kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ilipangiwa kiasi cha Shilingi Milioni928,594,224 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 imepatiwa Shilingi 608,220,329 (Mishahara 412,632,234 na Matumizi ya Kawaida 124,920,095 na ruzuku 70,668,000) sawa na asilimia 65.

39. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa kipindi cha mwaka 2024/2025, imetekeleza yafuatayo.

a) Afisi ilifanya kikao cha 44 cha Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu ambacho kilijadili mambo mbali mbali ikiwemo usimamizi na Uendeshaji wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu. Vilevile, Afisi imekamilisha maboresho ya mfumo wa kielectroniki wa kuhifadhia taarifa za Watu wenye Ulemavu (Jumuishi Management Information System) ambapo mfumo huo upo katika hatua za majaribio wa uingizaji wa taarifa za Watu wenye Ulemavu.

b) Afisi pia ilishiriki katika mafunzo ya siku mbili juu ya kutengeneza muongozo wa Kusimamia na kufundishia ujasiriamali. Lengo la mafunzo hayo ni kuwasaidia wajasiriamali wenye Ulemavu ili kuweza kuendeleza biashara zao na kujipatia fursa za masoko ili waweze kuuza bidhaa zao.

c) Afisi ilifanya ukaguzi wa Miundombinu rafiki kwa majengo 10 ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na matano ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kupitia ukaguzi huo ilibainika kuwa majengo 12 hayakuwa rafiki kwa Watu wenye Ulemavu na ushauri wa maboresho wa majengo hayo ulitolewa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

d) Afisi kwa kushirikiana na Madrasa Early Childhood Programme pamoja na Shirikisho la Jumuiya za Watu wenye Ulemavu (Shijuwaza), imewapatia mafunzo watu 36 (wanawake 13 na wanaume 23) ambao ni wajumbe wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na viongozi wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu kwa lengo la kuwapatia uelewa wajumbe hao juu ya dhana ya Ulemavu pamoja na mradi wa CBID.

e) Katika kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kumudu maisha yao ya kila siku, Afisi imetoa jumla ya vifaa saidizi 425 vyenye thamani ya shilingi 325,500,000 vikijumuisha viti 345 vya magurudumu mawili, viti 30 vya vya magurudumu mawili vya moto, fimbo nyeupe 50. Vile vile, kwa kushirikiana na Taasisi ya Annouryyakin foundation Afisi imewapatia ftari Watu wenye Ulemavu 1000 (wanawake 720 na wanaume 280) ikiwemo mchele kilo 5, unga kilo 5, sukari kilo 5, mafuta ya kupikia na chumvi kwa lengo la kuwawezesha na kuwajumuisha Watu wenye Ulemavu.

f) Afisi imeendelea kuwalipia gharama za masomo ya muda mfupi na muda mrefu wanafunzi 24 (wanaume 11 na wanawake 13) wenye Ulemavu katika fani mbalimbali kwa mwaka 2024/2025 ambapo mafunzo ya muda mrefu ni wanafunzi 20 (wanaume 11 na wanawake 9) na mafunzo ya muda mfupi ni wanafunzi 4 wanawake.

g) Afisi pia imeendelea kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kwa kuwapatia vifaa mbali mbali vikiwemo milango miwili ya geti, saruji mifuko 10 na magodoro mawili ili kujikimu katika maisha yao ya lazima.

h) Afisi imeendelea kukuza uelewa wa jamii juu ya masuala ya watu wenye ulemavu kwa kurusha hewani jumla ya vipindi 4 vya T.V (ZCTV na TBC) na vipindi 10 vya redio (ZBC redio vipindi 4, Habari FM 1, Bahari FM 2, Coconut FM 1, Crown redio 1 na Assalamu redio1). Vipindi hivyo vilizungumzia "Dhana ya Ulemavu", "Ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika kuelekea Uchaguzi" na "Kuelekea siku ya watu wenye ulemavu Duniani tarehe 3 Disemba".

i) Afisi pia imeandaa Bonanza la Michezo kwa watoto wenye Ulemavu, ambapo jumla ya watoto 100 (wenye ulemavu 50 na wasio na ulemavu 50) walishiriki ambapo wanawake 51 na wanaume 49 ikiwa ni miongoni mwa shughuli za shamrashamra za kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani tarehe 3 Disemba. Aidha, michezo

mbali mbali ilifanyika ikiwemo kuruka kamba, mbio za magunia, kuvuta kamba, kukalia viti na mchezo wa kuvuka vikwazo. Michezo hiyo ilifanyika katika viwanja vya Kisakasaka Wilaya ya Magharibi "B" wanafunzi kutoka skuli mbalimbali ziliweza kushiriki. Skuli zilizoshiriki ni Skuli ya Jan'gombe (Mjumuisho), Skuli ya Kisiwandui (Mjumuisho), Skuli ya Salum Turky, Skuli ya Jendele (Mjumuisho), Skuli ya Dr.Samia na Skuli ya Kisauni msingi.

j) Afisi iliadhimisha siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani tarehe 3 Disemba 2024 yaliyofanyika uwanja wa Gombani ya kale ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa. Othman Masoud Othman na kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa ni **"Kukuza uongozi wa Watu wenye Ulemavu kwa mustakbali Jumuishi na Endelevu".**

k) Afisi kwa kushirikiana na Zanzibar Initiative Oganization na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu ilifanya maonyesho ya siku 3 ya wajasiriamali wenye ulemavu katika viwanja wa Mapinduzi Square (Kisonge) ili kutoa fursa kwa Watu wenye ulemavu kutafuta masoko ya bidhaa zao na kutangaza shughuli mbalimbali wanazozifanya. Jumla ya vikundi 40 (22 vya wajasiriamali wenye ulemavu na vikundi 18 vya wajasiriamali wasio na ulemavu) vinavyojishughulisha na shughuli mbalimbali za ufinyanzi, ushoni na ufumaji vilishiriki maonyesho hayo.

**Programu Kuu: PB0104 Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza Wa Rais**

**Matokeo ya muda mrefu:** Upatikanaji wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais

40. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2024/2025 iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 2,747,561,460 (Mishahara Shilingi Milioni 673,031,460 na matumizi mengineyo Shilingi Milioni 574,530,000 na Shilingi Bilioni 1,500,000,000 kwa miradi ya maendeleo). Programu hii Kuu kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ilipangiwa kiasi cha Shilingi Milioni 937,717,640 mpaka kufikia mwezi Machi, 2025 imepatiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi 664,305,916 (471,681,496 Mishahara na Matumizi mengineyo 192,624,420) sawa na asilimia 71 ya utekelezaji programu.

41. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais imetekeleza yafuatayo: -

a) Afisi imeendelea kutoa huduma stahiki kwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais na kuratibu vikao vya mabalozi na wageni mbali mbali kwa ajili ya kuimarisha mahusaino na mashirikiano ambapo jumla ya wageni 604 wa ndani na nje wamepokelewa.

b) Vile vile, Afisi imeratibu safari na ziara mbali mbali za Mheshimiwa za ndani kumi na nne (14) na nje tatu (3) ya nchi ili kuona shughuli za Afisi zinatekelezwa kama zilivyopangwa.

c) Kero 129 kutoka kwa wananchi zimeendelea kupokelewa na kuzipatia ufumbuzi.

d) Kupitia kitengo cha habari taarifa na makala mbali mbali zinazohusiana na sekta ya mazingira, Watu wenye Ulemavu, UKIMWI, Dawa za kulevya na maelekezo juu ya utatuzi wa changamoto kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii

**Programu Ndogo SB010302: Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti**

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SB010302) ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti ina lengo la Kusimamia utekelezaji wa Mipango, Miradi ya maendeleo na Bajeti. Kwa mwaka 2024/2025 iliidhinishiwa Shilingi Milionin 355,058,957 (Mishahara Shilingi Milioni 167,658,957 na matumizi mengineyo Shilingi Milioni 187,400,000). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu imetengewa kiasi cha Shilingi 273,864,895. Hadi kufikia Machi, 2025 imepatiwa kiasi cha Shilingi 134,495,992 (Mishahara 100,562,100 na Matumizi mengineyo 33,933,892) sawa na asilimia 49.

43. **Mheshimiwa Spika, Programu hii imetekeleza yafuatayo:-**

a) Kuandaa ripoti za Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2023- 2024 na robo ya

kwanza kwa mwaka 2024-2025 zimeandaliwa na kuwasilishwa Tume ya Mipango na ripoti ya tathmini ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na mwelekeo kwa mwaka 2025-2030 pamoja na taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020-2025 kwa kipindi cha Novemba, 2023 hadi Ogasti, 2024 ziliandaliwa na kuwasilishwa.

b) Afisi kwa kushirikiana na Wataalamu imeandaa rasimu ya mpango wa utekelezaji na mpango wa ufuatiliaji wa Sera ya mazingira ambapo kwa sasa unakusudia kuwasilishwa kwenye kikao cha wadau wa utekelezaji.

c) Vilevile, Afisi imeratibu vikao vya kamati ya kuchunguza hesabu kuu za Serikali na Kamati ya Makatibu wakuu na Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi.

d) Afisi imewapatia mafunzo maafisa wa Idara na Taasisi zake wanaoshughulika na kazi za Mipango na Ufuatiliaji na Tathmini kwa miradi ya maendeleo, dhana ya Utafiti kwa kuzingatia mwongozo wa Tume ya Mipango. Aidha, vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi vimenunuliwa vikiwemo compyuta na projekta.

e) Afisi imekusanya Takwimu za kimazingira na za Watu Wenye Ulemavu kwa mwaka 2024 na kuziwasilisha Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya maandalizi ya kitabu cha takwimu (Zanzibar Statistical Abstract) kinachoandaliwa na kutolewa

kila mwaka. Afisi pia imeratibu mandalizi ya kikao kwa ajili kupokea maoni ya kamati ya Kanuni na sheria ndogo ndogo za Baraza la Wawakilishi juu ya kanuni za Watu Wenye Ulemavu na Kanuni ya matumizi salama na Bioteknologia

f) Idara imefanya ziara ya ufatiliaji wa miradi yote inayotekelezwa na Afisi ukiwemo mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi katika eneo la Sipwese ambapo ujenzi wa tuta umekamilika kwa asilimia 98. Aidha, ziara hiyo pia imefanyika katika ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji chumvi eneo la Kisiwa panza na kubaini kwamba tayari ukuta huo wenye urefu wa mita 70 umekamilika.

l) Afisi kwa kushirikiana na Afisi ya Waziri Mkuu (SJMT) imeratibu na kufanya kikao cha mashirikiano kwa lengo la kuleta ufanisi na kupata fursa zilizopo kwa ajili ya kuleta usawa kwa Watu wenye Ulemavu nchini.

m) Katika kuandaa na kufanya mapitio sera na sheria, Afisi imeendelea kufanya mapitio ya sera ya mazingira ya mwaka 2013 ambayo ipo katika hatua ya kuwasilishwa katika kikao cha kitaalamu cha Makatibu Wakuu. Aidha, kwa upande wa sera ya UKIMWI hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kikosi kazi na rasimu ya awali.

**Programu Ndogo SB010301: Utumishi na Uendeshaji**

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SB010301) ya Utumishi na Uendeshaji ina lengo la Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi na utoaji wa huduma za Afisi. Kwa mwaka 2024/2025 iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 1,679,095,076 (Mishahara Shilingi Milioni 922,195,076 na Matumizi mengineyo Shilingi Milioni 706,900,000). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu ilipangiwa Shilingi 1,274,535,717 hadi kufikia mwezi Machi, 2025 kiasi cha Shilingi 688,130,180 (Mishahara 495,352,547 na Matumizi mengineyo 192,777,633) sawa na asilimia 54 ya utekelezaji wa programu.

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

a) Afisi imekamilisha zoezi la mapitio ya mkataba wa utoaji huduma kwa mtaka huduma ambapo imejumuisha washiriki kutoka taasisi mbali mbali wakiwemo Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Asasi za Kiraia na umewasilishwa Afisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

b) Katika kuwajengea uwezo watumishi, Afisi imeendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi wake katika fani tofauti ambapo mtumishi mmoja kutoka Idara ya Utumishi na Uendeshaji ngazi ya shahada ya kwanza katika fani ya utawala wa rasilimali watu,

mmoja katika ngazi ya Diploma ya juu (PGD) na mtumishi mmoja kutoka Idara ya Mipango ngazi ya shahada ya pili katika fani ya sayansi ya uchumi na fedha. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi mtumishi mmoja amepatiwa mafunzo ya muda mfupi yanayohusiana na "Enhasing leadership Skills in managing procurement and supply chain practice".

c) Afisi imewapatia mafunzo watumishi wake watano ambapo mtumishi mmoja amepatiwa mafunzo ya kompyuta (computing program and design), mtumishi mmoja amepatiwa mafunzo ya ukaguzi, mtumishi mmoja amepatiwa mafunzo ya manunuzi na watumishi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya habari, mifumo na matumizi salama ya bioteknolojia. Vile vile, Afisi imewapatia wafanyakazi wake 35 mafunzo yanayohusiana na kukabiliana na maafa juu ya namna ya kutumia vizimia moto (fire extinguishers) pamoja na mafunzo ya Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma.

c) Ujenzi wa jengo dogo la vyumba vinne unaendelea katika eneo la Afisi ya Makamu wa Kwanza chini ya Mkandarasi Sarasaa ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 65. Aidha, uwekaji wa mfumo wa kuangalia usalama (CCTV Camera) umekamilika.

d) Vikao vitatu (3) vya kamati ya Wizara vya ukaguzi wa ndani na vikao kumi na mbili (12) vya bodi ya

zabuni ya Wizara na vikao vitatu (3) vya kamati ya uongozi wa Wizara vilifanyika.

e) Huduma mbali mbali za utawala na uendeshaji wa Afisi zimetolewa zikiwemo huduma ya umeme, maji, mafuta, vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi, usafiri, ziara na safari za viongozi, vikao mbali mbali, matengenezo ya vyombo vya usafiri na matengenezo madogo madogo ya Afisi. Afisi pia imeendelea kulipa stahiki mbali mbali za watumishi ikiwemo likizo ambapo jumla ya watumishi 7 (wanawake 3 na wanaume 4) wamelipwa stahiki zao. Aidha, watumishi 8 (wanawake 4 na wanaume 4) wamelipwa stahiki zao za malipo baada ya saa za kazi.

**Programu Ndogo SB010303: Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba**

**46. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SB010303) ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba ina lengo la Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi na utoaji wa huduma kwa Afisi kuu - Pemba. Kwa mwaka 2024/2025 iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 1,059,737,913 (Mishahara Shilingi Milioni 600,537,913 na Matumizi mengineyo Shilingi Milioni 459,200,000). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu imetengewa kiasi cha Shilingi Bilioni 1,009,021,436 hadi kufikia mwezi Machi, 2025 imepatiwa kiasi cha Shilingi 616,441,477 (shilingi 409,116,244 kwa ajili ya mishahara na shilingi

206,225,333 kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 61 ya utekelezaji wa programu.

47. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 kwa upande wa Pemba Programu imetekeleza yafuatayo:-

a) Imeendelea kusimamia shughuli zote ambazo zinatekelezwa na Idara za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

b) Afisi iliratibu ziara za Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais kisiwani Pemba kwa ajili ya kutembelea sehemu mbalimbali ikiwemo kukagua Shamba la Mikoko Sipwese kwa Mgogo Wilaya ya Mkoani, kukagua Vitalu vya Miche mbali kama vile Kitalu cha Chanjaani Meli mbili, Kitalu cha weni, Kitalu cha Konde, machimbo ya mali zisizorejesheka katika eneo la Pujini na uwondwe.

c) Afisi pia ilitowa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu katika ukumbi wa Tibirinzi ZSSF na kuratibu ziara za waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wakilishi pamoja na Viongozi Wakuu kutoka Afisi kuu Unguja.

d) Afisi pia iliratibu ugawaji wa Mitungi ya gesi 800 katika Shehia ya Kisiwa Panza, kilele cha maazimisho ya Watu wenye Ulemavu, maazimisho ya siku ya UKIMWI, makabidhiano ya Ujenzi wa ukuta wa kuzuiya Maji ya chumvi yasiingie katika mashamba ya wananchi huko Kisiwa Panza pamoja na kuratibu

kikao cha kutoa maoni juu ya kanuni za watu wenyenulemavu,

e) Afisi imeendelea kuimarisha mazingira bora ya kazi na upatikanaji vitendeakazi kwa kulipa stahiki za wafanya kazi kama vile kulipa mishahara, kulipa maji, umeme, Matengenezo ya Ukumbi, matengenezo ya kenop 5 za nyumba ya Makaazi ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, ununuzi wa fanicha za ukumbi, likozo 13, na mafunzo ya muda mfupi 4 na muda mrefu 7

**FUNGU B04 (USIMAMIZI WA MAZINGIRA)**

**PROGRAMU KUU PB0401: Usimamizi wa Mazingira Matokeo ya muda mrefu: Kuimarisha usimamizi wa mazingira**

**48. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cjha mwaka 2024/2025 Programu hii iliidhinishiwa shilingi 1,835,300,000 katika utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi 1,133,400,000 ni kwa ajili ya mshahara, na shilingi 701,900,000 kwa matumizi mengineyo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025 ilipangiwa Shilingi Bilioni 1,445,812,999 (Mishahara Shilingi Milioni 850,050,000 na matumizi mengineyo Shilingi Milioni 595,762,999). Hadi Machi, 2025, shilingi 1,445,812,999 zilipangwa kutumika ambapo jumla ya shilingi 1,057,056,597 (shilingi 729,463,431 kwa ajili ya mishahara na shilingi 327,593,166 kwa matumizi mengineyo) zilipatikana sawa na asilimia 73. **Kiambatanisho nambari 7A kinahusika.**

49. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SCB04101 na SCB04102) ya Tathmini na ufuatiliaji wa kimazingira na Uzingatiaji na utekelezaji wa sheria. Kwa kipindi cha mwaka 2024/2025, programu hii imetekeleza yafuatayo: -

a) Kusimamia marufuku ya mifuko ya plastiki kwa ajili ya kupunguza athari za kiafya na kimazingira zinazotokana na mifuko hiyo ambapo operesheni 54 zimefanyika, watu 101 wamekamatwa na jumla ya kilo 597 za mifuko ya plastiki. Watu hao wamefikishwa mahakamani na kutozwa faini ya shilingi 14,375,000 ambazo zimeingia kwenye mfuko mkuu wa mapato wa Serikali.

b) Kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka kwa kufanya jumla ya operesheni 45. Kwenye operesheni watu wanane (8) wamekamatwa na misumeno miwili ya moto imekamatwa Unguja na kutozwa faini ya jumla ya Shilingi 2,450,000. Aidha, kwa upande wa Pemba hakuna mtu aliyekamatwa na kuashiria kupungua kwa vitendo vya uchimbaji holela wa maliasili zisizorejesheka.

c) Kufanya ufuatiliaji wa maeneo 185 ya kimazingira kwa ajili ya kupunguza athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira (Kiambatanisho namba 1 kinahusika). Maeneo hayo yanatokana na mashimo ya mchanga, kifusi, mawe na matofali ya mawe pamoja na yenye usimamizi duni wa taka na uchafuzi wa mazingira unatokana na viwanda vya matofali ya mawe.

Kwenye ufuatiliaji huo miongozo ya kimazingira imetolewa ambayo imesaidia kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira wa maeneo hayo.

d) Kuhakikisha miradi ya kiuchumi na kimaendeleo inatekelezwa bila kuathiri mazingira, Afisi imeratibu jumla ya Tathmini za Kimazingira kwa miradi 102 ya kiuchumi na kimaendeleo na kupewa vyeti vya aina tofauti vya kimazingira **(Kiambatanisho namba 1 kinahusika)**. Masharti ya kimazingira yameambatanishwa na vyeti hivyo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa miradi hiyo inaendelezwa bila ya kuwa na uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira.

e) Kufuatilia miradi 213 ya kiuchumu na maendeleo Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakuwa endelevu bila ya kuleta athari kubwa za kimazingira na kijamii (Kiambatanisho namba 1 kinahusika). Wastani wa asilimia 85 ya miradi hiyo imeonekana kuzingatia masharti na miongozo ya kimazingira iliyotolewa na asilimia iliyobakia ya miradi ilipewa msisitizo wa kufuata masharti hayo.

f) Kukuza uelewa na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kupitia vipindi 5 vya redio na 3 vya TV pamoja na kutumia mitandao ya kijamii ili kuelimisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira. Aidha, idadi ya vipindi hivyo imepatikana kutokana na ZEMA kufanikiwa kuhamasisha upatikanaji wa vipindi vilivyokuwa havina malipo kutokaVituo

husika. Mada za vipindi hivyo zinaonekana katika **kiambatanisho namba 9 kinahusika.**

g) Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ ilitoa elimu ya usafi wa mazingira na katazo la mifuko ya plastiki kwa viongozi na wakuu wote wa masoko na kamati za masoko Unguja na Pemba. Jumla ya masoko 11 yalihusika ambapo Unguja ni masoko sita (6) na Pemba ni masoko Matano (5). Kwa upande wa Unguja ni soko la Samaki Malindi, soko la mboga mboga kwerekwe, soko la Jumbi, soko la Kinyasini, soko la Mkwajuni na soko la Mkokotoni. Kwa upande wa Pemba, masoko hayo ni soko la Mtambile, soko la Kivumbikae, soko la Tibirinzi Chakechake, soko la wajasiriamali kipitacho Mkoani na soko la Matunda Wete na jumla ya wafanyabiashara 300 wa masoko hayo walipatiwa elimu hiyo.

h) Afisi imewapatiwa jumla ya watumishi 11 (9 Unguja na 2 Pemba) walikwenda likizo na walilipwa posho za likizo; watumishi 3 wa Unguja walipatiwa mafunzo mafupi ya aina tofauti, watumishi 10 wamepandishwa madaraja ambapo Unguja 7 na Pemba 3, watumishi 2 wamebadilishwa kada, mtumishi 1 amethibitishwa kazini na watumishi 21 (16 Unguja na 05 Pemba) walipimwa utendaji kazi na kupata nyongeza za mshahara za mwaka (Annuall Increament). **Kiambatanisho namba 10B kinahusika.**

**FUNGU C04 (MAMLAKA YA UDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA)**

**PROGRAMU KUU PC0401: Udhibiti wa dawa za kulevya**

**Matokeo ya muda mrefu:** Jamii kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 Programu hii iliidhinishiwa shilingi 4,955,000,000. Kati ya fedha hizo shilingi 1,165,700,000 ni kwa ajili ya mshahara, shilingi 1,239,300,000 kwa matumizi mengineyo na shilingi 2,550,000,000 kwa kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025 ilipangiwa Shilingi Bilioni 1,759,475,000 (Mishahara Shilingi Milioni 874,275,000 na matumizi mengineyo Shilingi Milioni 885,200,000). Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya Shilingi Bilioni 1,121,679,306 (Matumizi ya Kawaida 441,582,581 na Mishahara 680,096,725 na shilingi Milioni 125,039,827 ni kwa ajili ya mradi wa maendeleo) zilipatikana sawa na asilimia 64. **kiambatanisho namba 7A kinahusika.**

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SC040101 na SC040102) ya Uchunguzi na Operesheni wa Dawa za Kulevya na Uhalifu unaofanana nao pamoja na Kinga, Tiba na Marekebisho ya Tabia ina lengo la kuzuia uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

52. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imetekeleza yafuatayo: -

a) Afisi imeendelea kufanya Operesheni za kuwakamata wahalifu wa dawa za kulevya ambapo kupitia operesheni hizo jumla ya kesi 107 (89 Unguja, 18 Pemba) zilifunguliwa. Operesheni hizo zilihusisha watuhumiwa 110 (wanaume 102 na wanawake 8) wanaojihusisha na shughuli za usambazaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

b) Afisi inaendelea kuhakikisha watuhumiwa wa kesi za dawa za kulevya wanafikishwa katika vyombo vya sheria na kuwafungulia kesi Mahkamani, katika kutekeleza hilo, kesi 72 (kesi 49 huru na kesi 23 hatia) zimetolewa hukumu na kesi 171 bado zinaendelea Mahakamani.

c) Afisi imefanya zoezi la kuteketeza vielelezo vya kesi za Dawa za Kulevya vilivyo hifadhiwa katika sehemu za kisheria ambazo ni Mahakama, Vituo vya Polisi na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba. Jumla ya kg 1,619.86 ziliteketezwa.

d) Afisi imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya pamoja na Sheria Nambari 8 ya 2021 katika maeneo mbali mbali ikiwemo taasisi za elimu, masheha, wananchi, vikosi vya Ulinzi na Usalama na maeneo ya kazi kwa Unguja na Pemba. Elimu hiyo ilitolewa kupitia ZBC TV na ZBC Radio

e) Mamlaka imeendelea na kazi ya kutoa elimu ya athari dhidi ya dawa za kulevya kwa jamii Unguja na Pemba, ambapo jumla ya wanafunzi 7,343 (wanaume 3228 na wanawake 4,115) na walimu 71 walipatiwa elimu kutoka skuli mbali mbali. Aidha, shehia za Bumbwini, Langoni, Marumbi, Mpapa, Muyuni, Mahonda, Gana na Donge, Amani (Unguja) na Shehia za Wesha, Gando, Mchanga Mrima, Mbuzini, Vitongoji na Ngwachani (Pemba) zilifikiwa na jumla ya wananchi 1139 (wanaume 625, wanawake 514) walipatiwa elimu. Pia elimu ilitolewa kupitia vyombo vya habari na vipindi 6 vilirikodiwa na kurushwa hewani kupitia Zanzibar Cable Television, Bahari FM Redio na ZBC TV kuhusiana na sheria Nam.8 ya 2021, athari pamoja na uhalifu wa dawa za kulevya. Elimu hii imewasaidia jamii hasa wanafunzi kufahamu dawa za kulevya, athari zake na kuweza kujiepusha na usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya pamoja na kutoa taarifa za uhalifu kwa vyombo vinavyohusika.

f) Afisi imeendelea kutoa huduma za tiba na marekebisho ya tabia kwa vijana waliaoachana na matumizi ya Dawa za Kulevya katika Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni ambapo katika kipindi cha Julai – Machi, 2024 jumla ya waraibu 104 wamepokelewa na kupatiwa huduma za tiba, marekebisho ya tabia, elimu ya ushauri nasaha pamoja na kujifunza kazi za ujasirimali. Aidha, Afisi imewapima afya waraibu katika vituo kwa kuwafanyia

vipimo vya maradhi mbali mbali yakiwemo vipimo vya HIV/AIDS, Homa ya Ini B na C, Kaswende, Malaria na Kisukari na waliobainika na tatizo kupatiwa tiba stahiki. Jumla ya waraibu 46 walifanyiwa vipimo hivyo na waraibu 14 waligundulika na magonjwa ya akili na waraibu 4 kugundulika na Homa ya Ini C.

g) Tiba ya kifamilia (Family Therapy) imefanyika kwa wazazi wa familia 77 za waraibu wanaopata huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu. Lengo ni kujadili maendeleo ya vijana hao pamoja na njia bora za kuishi nao mara watakapomaliza huduma za tiba na kuweka mikakati ya kutorudia matumizi ya dawa za kulevya na kuisaidia Serikali katika kupiga vita uhalifu wa dawa za kulevya nchini.

h) Afisi imezingatia umuhimu mkubwa wa kujenga uwezo watendaji ili kuleta tija na ufanisi katika utendaji wa kazi kwa kuwapatia mafunzo ambapo watendaji 75 (25 Unguja na 50 Pemba) wamepatiwa mafunzo juu ya kubaini, kuchunguza na kuendesha mashtaka yanayohusiana na makosa ya utakatishaji fedha haramu na uhalifu wa kupangwa kupitia Mradi endelevu wa kupambana na rushwa na uhujumu uchumi (BSAAT).

**53. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu ina lengo la kuweka mazingira mazuri ya kazi na kuendesha shughuli za Mamlaka.

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

a) Afisi imelipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo mishahara, malipo ya likizo pamoja na kugharamia huduma za usafiri. Aidha, gharama za umeme, magazeti ya Serikali, safari za kikazi zimelipiwa kwa Unguja na Pemba kwa ajili ya kuweka mazingira bora ya kazi yenye kuleta ufanisi. Afisi imefanya Kikao cha Pili cha Baraza la Taifa la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

b) Afisi imeendelea kushiriki vikao mbali mbali vikiwemo vikao vya kukuza mashirikiano baina ya taasisi za haki jinai, Mamlaka ya Bahari Kuu, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa lengo la kuondoa migongano ya Sheria na Kanuni, kujadili changamoto pamoja na kutoa mapendekezo juu ya uendeshaji wa kesi zenye kipaombele (high profile cases). Mheshimiwa Spika, Afisi imeratibu ziara mbili za Kamati ya Baraza la Wawakilishi ambazo ni kutembelea Afisi ya Mamlaka ya Dawa za Kulevya Tanzania Bara (DCEA) kuweza kujengeana uwezo na kupata uzoefu wa kujifunza uchunguzi wa sayansi ya jinai (Forensic investigation). Pia, kutembelea eneo linalotarajiwa kujengwa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kangagani – Pemba. Pia, Afisi imesaini hati ya Makubaliano ya utendaji kazi kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania Bara na Zanzibar.

c) Afisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Zanzibar Opportunity Institute (ZOI) imeandaa Tamasha la kupiga vita matumizi na usafirishaji wa Dawa za kulevya kwa lengo la kuihamasisha jamii kuachana na matumizi ya Dawa za kulevya kwa kushiriki katika michezo na burudani mbali mbali ambapo zaidi ya watu 2000 walijumuika katika Tamasha hilo.

d) Afisi kwa upande wa miradi ya maendeleo imeanza hatua za utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Pemba ambapo hadi sasa hatua za awali za ujenzi zimeanza ikiwemo utayarishaji wa michoro ya kituo, makisio ya ujenzi, tathmini ya kimazingira na utafiti wa udongo katika eneo la mradi Kangagani Pemba yamekamilika ambapo ujenzi wa kituo hicho utafanywa na makandarasi JKU chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo Zanzibar.

**FUNGU C05: TUME YA UKIMWI**

55. **Mheshimiwa Spika,** fungu hili lina programu kuu mbili kama ifuatavyo:-

**Programu Kuu C0501: Programu Kuu ya Kuratibu Mwitiko wa Taifa Wa UKUMWI**

**Matokeo ya muda mrefu:** Kiwango cha maambukizo ya VVU kupungua kutoka 0.4% hadi 0.2 ifikapo 2030 nchini.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii iliidhinishiwa shilingi 2,000,686,000 katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo shilingi

761,300,000 kwa ajili ya mishahara na 1,239,386,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025 ilipangiwa Shilingi Bilioni 1,36,699,984 (Mishahara Shilingi Milioni 761,299,992 na matumizi Mengineyo Shilingi Milioni 575,399,992). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya shilingi 746,192,169 (Mishahara ni shilingi 472,445,659 na Matumizi ya Kawaida ni shilingi 273,746,510) zilipatikana sawa na asilimia 56 kwa ajili ya utekelezaji wa programu zake ndogo. **Kiambatanisho namba 7A kinahusika**.

57. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imetekeleza yafuatayo:-

a) Tathmini ya mwitiko wa UKIMWI imefanyika na kuonesha kwamba hadi kufikia Disemba 2024, jumla ya watu 10,645 wanakisiwa kuishi na Virusi vya UKIMWI. Kati yao watu 9,799 tayari wamesajiliwa katika kliniki za matibabu ambapo (wanawake 6,783 na wanaume 3,016). Miongoni mwa watu waliosajiliwa kwenye kliniki hizo, watu 9,524 tayari wameanzishwa dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI (wanawake 6,586 na wanaume 2,938), wamesajiliwa katika kliniki za tiba ambapo (wanawake 6,783 na wanaume 3,016). Idadi hiyo inaonyesha kwamba, kiujumla kuna ongezeko la watu wanaoambukizwa kutoka 257 mwaka 2023 na kufikia watu 362 mwaka 2024. Katika mwaka huu wa fedha, Afisi imekamilisha mapitio ya Mkakati wa Kitaifa wa Kondomu (2024-2029) ili kuhakikisha

unaenda sambamba na Mkakati wa Nne wa Taifa wa UKIMWI. Mkakati huu unalenga kuimarisha juhudi za kuzuia maambukizo ya VVU kwa kuhakikisha upatikanaji na matumizi sahihi ya kondomu ikiwa ni njia kubwa ya kitaalamu inayoweza kuzuia maambukizo ya VVU yasiendelee. Hatua inayofuata ni kuuchapisha na kuufikisha kwa taasisi mbalimbali na wadau kwa ajili ya utekelezaji.

b) Afisi imefanya mikutano nane (8) ya kuratibu na kuandaa kwa kuzishirikisha taasisi zinazohusika na utekelezaji wa programu mbalimbali zinazohusiana na UKIMWI ili kuangalia utekelezaji, ufanisi na changamoto katika utekelezaji wa programu mbalimbali. Mikutano hiyo ilihusu huduma jumuishi za UKIMWI na afya ya uzazi, uratibu wa kuangalia utekelezaji wa Maazimio ya ESA (East and Southern Africa), uratibu wa programu ya ONGEA msimu wa Pili, uratibu wa wadau wanaofanya kazi na makundi maalum, uratibu wa kuangalia utekelezaji wa Maazimio ya ESA (East and Southern Africa), uratibu wa programu ya ONGEA msimu wa Pili na uratibu wa wadau wanaofanya kazi na makundi maalum.

c) Afisi ilitoa elimu ya VVU na UKIMWI na kuhamasisha jamii juu ya utumiaji wa huduma za UKIMWI kupitia sherehe za kitaifa za maonesho ya kilimo ya nane nane na Mapinduzi yaliyofanyika Chamanangwe Pemba na Nyamanzi Unguja kwa mfuatano huo. Jumla ya vipeperushi 317, majarida 32, vifaa 101

vya JIPIME na kondomu za kiume 2,160 viligaiwa kwa watu wenye uhitaji katika maonesho hayo. Halikadhalika, elimu iliendelea kutolewa kupitia mitandao ya kijamii nayo ni YouTube, Instagram na facebook. Vile vile, jumla ya watu 4,549 wamepata elimu mbalimbali kupitia mitandao ya kijamii ya Afisi. Aidha, Afisi imetoa elimu na huduma za VVU kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Unguja na Pemba kupitia mijadala na huduma za masafa. Vyuo vilivyoshiriki ni Chuo Kikuu cha Taifa Tunguu, Karume Institute of Science and Technology (KIST), Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Chuo cha Utawala wa Umma (IPA), Zanzibar Business School (ZBS), Chuo cha Afya Mbweni, na Chuo cha Kiislamu kwa upande wa Unguja na Chuo cha Mwalimu Nyerere kwa upande wa Pemba.

d) Afisi imeandaa Jarida la Jihadhari toleo nambari 25 lenye Makala zinahusu elimu ya masuala mbalimbali juu VVU na UKIMWI, ikiwemo kuhamasisha matumizi ya huduma na matukio mbalimbali yanayohusu muitiko wa UKIMWI. Jumla ya majarida 200 yamechapishwa na kusambazwa sehemu mbalimbali kwa ajili ya kueneza elimu ya UKIMWI na masuala yanayohusiana nayo.

e) Afisi pia imefanya mafunzo ya siku mbili kwa waelimishaji rika 50 kutoka katika makundi ya waendesha boda-boda, wavuvi kutoka kambi za uvuvi (dago), wanafunzi wa vyuo vikuu, wafanyakazi

wa sekta ya uvuvi, wanawake wanaofanya biashara ya ngono, wanaume wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja, watu wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano, na wawakilishi wa vijana kutoka Mabaraza ya vijana. Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uelewa kuhusu njia za kujikinga na VVU, ikiwa ni pamoja na dawa kinga (PrEP), matumizi ya kondomu, huduma za afya ya uzazi na upimaji wa VVU ili waweze kusambaza taarifa sahihi. Aidha, vipeperushi 200 vilisambazwa kwa washiriki ili kuwasaidia katika kutoa elimu kwa wenzao.

f) Afisi imefanya ziara na vikao vya Kamati ya ukaguzi kwa kila robo mwaka ya utekelezaji kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025. Aidha, imefanya vikao vya Bodi ya Zabuni kwa lengo la kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2023-2024, kuidhinisha mpango wa manunuzi kwa mwaka 2024-25 na watoa huduma mbalimbali za Afisi kwa mwaka husika. Pia, Afisi imefanya vikao vya Bodi ya Makamishna. Vikao vyote hivi vililenga kusimamia uwajibikaji katika utendaji kazi na matumizi ya fedha za Serikali kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo.

g) Afisi imeimarisha matumizi ya mifumo ambayo ni e-Office, Mfumo wa barua pepe, mfumo wa rasilimali watu, mfumo wa bima ya afya na matumizi ya mitandao ya kijamii ya Afisi katika utoaji wa elimu. Afisi pia imeandaa Mkakati wa VVU na UKIMWI wa Vyuo vya Mafunzo kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma

ndani ya vyuo vya mafunzo kwa wanafunzi wakati wakiwa kifungoni na kuweka utaratibu utakaowasaidia kuendelea kupata huduma hizo watakapomaliza muda wao na kurudi uraiani.

h) Afisi iliwasilisha kwa wadau Miongozo iliyoandaliwa mwaka 2023-24 kupitia mikutano na wadau mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha utekelezaji wake ambapo wawakilishi 107 kutoka Sekta za Serikali, Mashirika ya Umma, Asasi za Kiraia, Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wahudumu wa Afya, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Viongozi wa Dini walishiriki mikutano miwili ya kuwasilisha Mkakati wa Nne wa Taifa wa UKIMWI Unguja na Pemba ambao ndio dira katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Aidha, Afisi iliwasilisha Muongozo wa Uzingatiaji wa Masuala ya UKIMWI kwa Taasisi 80 za Serikali yakiwemo Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mikoa, na zisizo za Serikali za Unguja na Pemba kwa lengo kuu la Muongozo huu ni kuelekeza namna taasisi hizo zinavyoweza kuzingatia masuala ya UKIMWI ndani na nje ya taasisi zao.

i) Afisi imelipa mishahara na stahiki za wafanyakazi pamoja na kulipa kodi ya jengo la Afisi na ununuzi wa huduma za maji, umeme, mafuta, matengenezo na ulinzi. Pia imenunua vifaa vya Afisi na matumizi mengineyo ikiwemo kompyuta kwa lengo la kuleta ufanisi. Aidha, Afisi iliendelea kugharamia

masomo ya muda mrefu kwa wafanyakazi watano (5) katika ngazi ya shahada na uzamili. Kati yao, wafanyakazi wanne wameshamaliza masomo yao. Vilevile, Watumishi wawili (Afisa Utumishi na Afisa Kumbukumbu) wamepata mafunzo yanayohusiana na utendaji sahihi, kanuni na sheria katika usimamizi wa kumbukumbu za kielektroniki na Wafanyakazi wawili (Afisa Utumishi na Afisa Utawala) walishiriki mafunzo kazi yanayohusiana na Human Resource and Payroll System na Afisa Manunuzi mmoja alipata mafunzo ya uingizaji wa mali za taasisi katika mfumo (ZGAMIS).

## MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

58. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inasimamia mafungu makuu ya kibajeti manne (4) ambayo ni B01 – Fungu la Afisi wa Makamu wa Kwanza wa Rais (Afisi kuu); B04 – Fungu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira; C04 – Fungu la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na C05 – Fungu la Tume ya UKIMWI.

59. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 itatekeleza Bajeti ya Programu (PBB) kupitia programu zake kuu saba (7) ambazo ni:-

i. Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi;

ii. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;

iv. Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya;

v. Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI;

vi. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; na

vii. Programu ya Usimamizi wa Mazingira

60. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi mitano (5) ya maendeleo kama ifuatavyo:-

i. Mradi wa kuirithisha Zanzibar ya kijani unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

ii. Mradi wa kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za pwani ya Zanzibar unaofadhiliwa na Adaptation Fund;

iii. Mradi wa usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika;

iv. Mradi wa ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

v. Mradi wa Kuimarisha mifumo ya Kitaifa na kuziwezesha Serikali za Mitaa kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi (SCALE) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano 2025/2030 ambapo jumla shilingi 317,680,000,000 zimetengwa kwa Wilaya 56 za Tanzania (45 Tanzania Bara na 11 Zanzibar).

61. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendeleza mashirikiano na Taasisi mbali mbali zikiwemo UNOPS, UNDP, IOC, Taasisi ya Uongozi Tanzania na Asasi za kiraia (NGO) ya CAN-TZ katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na watu wenye ulemavu kama ifuatayo:-

i. Mradi wa kuzuia maji ya Bahari katika eneo la Tovuni-Pemba na Bumbwini-Unguja.

ii. Mradi wa uhimilivu na uhifadhi wa bioanuwai katika Kisiwa cha Tumbatu-Unguja.

iii. Mradi wa uhimilivu wa mifumo ikolojia ya baharini na pwani kwa jamii za wavuvi katika eneo la kusini mashariki-Pemba.

iv. Mradi wa kufanya uchunguzi wa watoto wakiwa na umri wa kuwa shuleni wenye matatizo ya uwoni na usikivu.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KWAKA WA FEDHA 2025/2026.

### Makadirio ya Mapato.

62. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS 700,801,000 kupitia vianzio vyake viwili (2) vya ada ya uhifadhi wa mazingira na ada ya ukaguzi wa mazingira viliopo Unguja na Pemba. **Kiambatanisho nambari 11 kinahusika.**

### Makadirio ya Matumizi kwa Programu kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

63. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naiomba Kamati yako iidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni 27,182,108,000. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 14,768,911,295 kwa matumizi mengineyo ambapo shilingi 6,941,400,000 ni Mishahara; Shilingi 5,883,411,295 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na ruzuku ya shilingi Bilioni 1,944,100,000 ambapo Shilingi 1,294,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 650,100,000 kwa ajili ya Mishahara. Pia, Afisi inaiomba Kamati yako iidhinishe jumla ya Shilingi 12,413,196,705 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (shilingi 10,000,000,000 kutoka SMZ na shilingi 2,413,196,705 kutoka kwa washirika wa maendeleo). Kwa ufafanuzi zaidi kuhusiana na makadirio ya matumizi rejea **kiambatanisho nambari 12 kinahusika.**

**64. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu saba (7) kama ifuatavyo:-

i. Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 6,837,611,000;

ii. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 1,944,100,000;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 2,955,689,000;

vi. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 1,239,836,000;

v. Programu ya Usimamizi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 3,085,100,000.

vi. Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 8,740,600,000; na

vii. Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 2,379,172,000;

## MALENGO YA PROGRAMU ZA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itatekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kutekeleza miradi ya kimazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na utekelezaji wa mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani.

ii. Kutayarisha ripoti ya Tathmini ya Kimazingira kwa kipindi cha miaka mitano (5) 2020/2025.

iii. Kufanya Tathmini na Kuandaa Mpango Mkakati mpya wa Mazingira

iv. Kuendeleza Mapambano dhidi ya dawa za Kulevya na kuimarisha utoaji wa huduma za Tiba na Marekebisho ya Tabia.

v. Ujenzi wa Kituo cha wanawake cha Tiba na marekebisho ya Tabia Kangagani Pemba pamoja na kuendeleza miradi ya ujasiriamali kwa waraibu.

vi. Kukuza uwezeshaji, ujumuishwaji na upatikanaji wa haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Maendeleo.

vii. Kutayarisha na kutekeleza Miongozo 2 na Mikakati 2 ya masuala Watu wenye Ulemavu.

viii. Kuwatambua watu wenye ulemavu nchini kwa kuwasajili katika mfumo wa Kidigitali wa kuhifadhia taarifa za watu wenye ulemavu.

ix. Kuratibu utekelezaji wa mkakati wa IV wa UKIMWI ili kudhibiti maambukizo mapya ya UKIMWI kwa vijana, makundi maalumu na jamii kwa ujumla

x. Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano na Utetezi wa UKIMWI kwa vijana kwa kuanzisha Mkakati wa Nne waTaifa wa UKIMWI, miongozo ya kitaifa na kisheria ya UKIMWI.

xi. Kuratibu na kutekeleza shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kuimarisha mashirikiano ya Kimataifa, Kikanda na kisekta baina ya SMZ, SJMT na wadau.

**Programu Kuu: Usimamizi wa mazingira na uhimili wa mabadiliko ya Tabianchi.**

66. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu Kuu ya Usimamizi wa mazingira na uhimili wa mabadiliko ya Tabianchi inaombewa jumla ya TZS 6,837,611,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 421,286,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 502,889,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 5,913,436,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo (4,500,000,0000 kutoka kwa SMZ na 1,413,436,000 kutoka kwa washirika wa Maendeleo.)

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kutayarisha Kanuni na Miongozo ya Kimazingira, Kufanya tathmini ya bioanuai Unguja, Kufanya vikao vya kamati ya ushauri, kamati ya ufundi ya mabadiliko ya tabianchi na kamati ya uongozi ya mabadiliko ya tabianchi,

ii. Kufanya utafiti wa kutambua maeneo yalioathirika na mabadiliko ya tabianchi Pemba pamoja na Kufanya utafiti wa mabwawa ya asili na michirizi ya maji katika maeneo mbalimbali ya Pemba,

iii. Kufanya tathmini juu ya wanyama adimu wanaopatikana Pemba pekee,

iv. Kukuza uelewa kwa jamii juu ya maswala ya mazingira na Mabadiliko Tabianchi kupitia Vipindi vya redio, TV na mikutano ya ushajihishaji kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na jamii,

v. Kufanya mkutano wa mashirikiano baina ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Afisi ya Makamu wa Rais na Mazingira,

vi. Ujenzi wa kuta/matuta katika maeneo ya fukwe ili kuzuia maji ya bahari kuingia katika maeneo ya kilimo na makaazi kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na kuendelea na Utekelezaji wa Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani.

**Programu Kuu: Usimamizi wa masuala ya Watu wenye Ulemavu.**

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaombewa TZS 1,944,100,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 650,100,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,294,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

69. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:

    i. Kuwajengea uwezo watendaji wake kwa kushirikiana na wadau mbali mbali, kutayarisha na kuweka miongozo (manuals) itakayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya baraza,

    ii. Kuingiza taarifa za Watu wenye ulemavu katika mfumo wa kuhifadhia taarifa za Watu wenye Ulemavu Unguja na Pemba,

    iii. Kuwezesha na kuwajengea uwezo watu wenye Ulemavu, Kuratibu na kuandaa maadhimisho ya Siku ya watu Wenye Ulemavu duniani,

    iv. Kushiriki vikao mbali mbali vya mashirikiano baina ya SMZ na SMT, Kuwapatia vifaa saidizi Watu Wenye Ulemavu,

v. Kuwajengea uelewa watu Wenye Ulemavu na jamii kuhusu masuala ya Watu Wenye Ulemavu na Kuendeleza mapambano dhidi ya udhalilishaji waWatu Wenye Ulemavu

**Programu Kuu: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza Wa Rais.**

70. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza Wa Rais inaombewa jumla ya TZS 1,239,836,000 kati ya fedha hizo, shilingi 752,709,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 487,127,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kuhudumia safari za ndani na nje ya nchi,

ii. Kuimarisha huduma za usafiri, Ununuzi wa vifaa na huduma ya mawasiliano,

iii. Kuimarisha huduma za wafanyakazi,

iv. Ununuzi wa vifaa vya kompiyuta na kuandikia,

v. Mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu,

vi. Matengenezo madogo madogo na huduma ya nyumba ya VP1

vii. Kupokea na kufuatilia utatuzi wa kero mbalimbli kwa Wananchi.

**Programu Kuu: Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza Wa Rais.**

72. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza Wa Rais inaombewa jumla ya TZS 2,955,689,000 kati ya fedha hizo, shilingi 1,654,305,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,301,384,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Programu ndogo: Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti**

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, sera na utafiti inaombewa jumla ya TZS 355,560,000 kati ya fedha hizo, shilingi 169,630,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 185,930,000 kwa ajili ya mishahara.

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kuratibu maandalizi ya mipango na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Idara,

ii. Kuratibu na kufanya tafiti za Afisi juu ya dawa za kulevya na Watu Wenye Ulemavu,

iii. Kuratibu mashirikiano ya kisekta baina ya SMZ, SJMT, mikutano ya kikanda na Kimtaifa
iv. Kufanya Ufuatiliaji na tathmini juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kazi za kawaida,
v. Kujenga uwezo na kuweka mazingira bora ya kufanya kazi.

**Programu ndogo: Utawala na uendeshaji**

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo ya Utawala na uendeshaji inaombewa jumla ya TZS 1,534,843,000 kati ya fedha hizo, shilingi 742,412,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 792,431,000 kwa ajili ya mishahara.

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kuratibu mafunzo kwa watendaji wa Wizara,
ii. Kuufanyia mapitio mkataba wa utoaji wa huduma kwa mtaka huduma,
iii. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi kwa ununuzi wa vifaa na ukarabati wa miundo mbinu, ununuzi wa vitendea kazi vya Afisi, kuwapatia watendaji stahiki zao,
iv. Kuwezesha mikutano ya Bodi ya Zabuni, Kamati Tendaji, Kamati ya Uongozi na Kamati ya Ukaguzi na Kutekeleza shughuli za kitengo cha sheria, ICT

na Habari cha Wizara, kurusha hewani vipindi vya redio na televisheni.

**Programu ndogo: Uratibu wa Afisi Kuu – Pemba**

**77. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo ya Uratibu wa Afisi Kuu – Pemba inaombewa jumla ya TZS 1,065,286,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 389,342,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 675,944,000 ni kwa ajili ya mshahara.

**78. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kuendelea kuratibu ziara za viongozi wakuu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza Pemba pamoja na shughuli zote zilizopo chini ya taasisi za Afisi ya Makamu wa kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba.

ii. Kuhamasisha taasisi za Serikali na NGO's pamoja na wadau wa maendeleo katika upandaji wa miti ili kuimarisha Zanzibar ya kijani.

iii. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Raisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

iv. Kuendelea kuboresha majengo ya Afisi, makaazi ya Makamu wa kwanza wa Rais Pemba na kusimamia miradi mbali mbali inayotekelezwa kisiwani Pemba.

v. Kuendelea kulipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo mishahara, likizo, maposho na ada za wafanyakazi ambao wapo masomoni.

vi. Kuratibu maadhimisho ya taasisi ambazo zipo chini ya Afisi ya Makamu wa kwanza wa Raisi kama vile Siku ya UKIMWI, Siku ya Mazingira, Siku ya Watu wenye ulemavu na Siku ya Dawa za kulevya.

**Fungu B04 (Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira)**

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inakusanya mapato kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa mwaka 2025/2026 imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 700,801,000 ambazo zinatokana na ada ya uhifadhi na ada ya ukaguzi wa mazingira kwa ajili ya kuchangia mapato ya Serikali. (**Kiambatanisho nambari 11 kinahusika**).

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Fungu B04 ili liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 3,085,100,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 736,900,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 1,196,100,000 ni kwa ajili ya mshahara pamoja na shilingi 1,152,100,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**81.** **Mheshimiwa Spika,** Mgawanyo wa fedha hizo kwa Programu za fungu la B04 (Mamlaka ya Usimamizi wa

Mazingira) inayojumuisha Programu kuu ya Usimamizi wa Mazingira na Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji ambapo Programu kuu ya Usimamizi wa Mazingira ni Shilingi 1,297,491,000 ambapo shilingi 145,391,000 matumizi mengineyo na 1,152,100,000 ni kwa ajili ya maendeleo. Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji Programu Kuu ni Shilingi 1,787,609,000 ambapo shilingi 591,509,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 1,196,100,000 ni kwa ajili ya mishahara.

82. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026, Afisi kupitia programu hizi imejipangia shabaha zifuatazo:-

i. Kuendeleza kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni, viwango na miongozo ya kimazingira;

ii. Kuhakikisha kuwa miradi yote ya kiuchumi na kimaendelea inayoanzishwa inafanyiwa tathmini za kimazingira ili kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu bila ya kusababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

iii. Kufanya ufuatiliaji wa kimazingira kwenye miradi na maeneo mbali mbali ya kimazingira utakaosaidia kupatikana kwa usimamizi endelevu wa mazingira,

iv. Kuendeleza elimu ya mazingira kwa jamii,

v. Kusimamia shughuli za uendeshaji wa Afisi pamoja na kuwa na watumishi ambao wanatekeleza majukumu yao kwa uweledi na ufanisi.

## Fungu C04 (Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya)

**83. Mheshimiwa Spika,** fungu C04 ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naiomba Baraza lako iidhinishe jumla ya Shilingi 8,740,600,000 ambapo shilingi 2,133,800,000 kwa ajili ya mishahara, Shilingi 2,106,800,000 kwa ajili ya matumizi ya mengineyo na shilingi 4,500,000,000 kwa ajili ya kutekeleza kazi za maendeleo.

**84. Mheshimiwa Spika,** Mgawanyo wa fedha hizo kwa Programu za fungu la C04 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya) inayojumuisha Programu kuu ya Udhibiti wa dawa za kulevya na Programu Kuu ya Utawala na Rasilimali watu ni kama ifuatavyo:- Shilingi 809,132,000 ni Matumizi ya kawaida na shilingi 4,500,000,000 miradi ya maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Udhibiti wa dawa za kulevya, shilingi 1,297,668,000 ni kwa matumizi ya kawaida na shilingi 2,133,800,000 ni mishahara kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Utawala na Rasilimali watu.

**85. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii, Afisi imepanga kutekeleza shabaha zifuatayo:-

i. Kufanya Operesheni kubwa na zakawaida, Kuteketeza dawa za kulevya,

ii. Kufanya Vikao vya wadau wa sheria,

iii. Kufanya mikutano ya Tiba za kifamilia,

iv. Kuzipatia ruzuku nyumba za upataji nafuu,

v. Kujenga kituo cha Tiba na marekebisho ya Tabia Pemba,

vi. Uendeshaji wa shughuli za Afisi,

vii. Kutoa elimu ya Athari za matumizi ya dawa za kulevya na

viii. Kuendeleza huduma za Tiba ma Marekebisho ya Tabia

**Fungu C05 (Tume ya UKIMWI**

**86. Mheshimiwa Spika,** fungu C05 ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako iidhinishe jumla ya Shilingi 2,379,172,000 ambapo shilingi 783,200,000 kwa ajili ya mishahara, Shilingi 748,311,295 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 847,660,705 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

**87. Mheshimiwa Spika,** Mgawanyo wa fedha hizo kwa Programu za fungu la C05 (Tume ya UKIMWI) inayojumuisha Programu kuu ya Kuratibu muitiko wa Taifa wa UKIMWI inaombewa shilingi 849,192,000 ambapo 179,676,295 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 669,515,705 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji inaombewa shilingi 1,529,980,000 ambapo shilingi 783,200,000 kwa ajili ya mishahara, shilingi 568,635,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 178,145,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia programu hii, Afisi imepanga kutekeleza shabaha zifuatazo:-

i. Kufanya midahalo, mikutano, machapisho, programu za mitandao ya kijamii na redio ili kuongeza uelewa wa masuala ya UKIMWI kwa vijana,

ii. Kuratibu wadau wanaotekeleza Mkakati wa Nne waTaifa wa UKIMWI katika ngazi zote,

iii. Kuuwasilisha Muongozo wa Uzingatiaji wa masuala ya UKIMWI kwa sekta zinazoandaa na kutekeleza miradi ya maendeleo,

iv. Kufanya ufuatiliaji wa miradi na mikutano ya kuratibu ya watekelezaji wa miradi yenye mipango ya UKIMWI,

v. Kuwapatia watendaji mafunzo kazi, kulipa mishahara na maslahi ya wafanyakazi, Kununua vifaa vya kazi na Afisi, kununua vifaa na kuendelea kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wafanyakazi,

vi. Kufanya mapitio ya Sera yaTaifa ya UKIMWI, na Sheria ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI ,

vii. Kutekeleza na kuratibu Mpango wa Uendelevu wa Muitiko wa Taifa wa UKIMWI nchini (Sustainability Plan),

viii. Kufanya utetezi wa kuweka muongozo wa VVU na UKIMWI katika sekta ya utalii,

ix. Kukusanya taarifa za wadau wanaotekeleza programu za UKIMWI kwa kutumia mfumo wa TEHAMA na kutoa ripoti pamoja na

x. Kufanya utafiti unaohusiana na masuala ya UKIMWI ili kuimarisha mipango ya baadae.

## SHUKURANI

**89. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo hayo, natumia fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako Tukufu. Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, inatanguliza shukurani zake za dhati kwa mashirikiano mazuri kupitia Taasisi mbali mbali zinazofanya kazi kwa pamoja zikiwemo Taasisis za Seriakali, Taasisi binafsi, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za kifedha, Asasi za kiraia pamoja Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Jamii kwa ujumla. sana wahusika wote waliochangia kufanikisha utendaji wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Afisi inaanza kwa kuzishukuru Taasisi za kiserikali zikiwemo, Afisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Afisi ya Waziri Mkuu, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwezekazaji, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wizara ya Mawasiliano Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo, Wizara ya Maji Nishati na Madini, Wizara ya Ardhi Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Afya na Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Vile vile, tunazishukuru Taasisi na Mashirika zikiwemo Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Kudhibiti na

Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania, ZBA, ZPDB, ZAECA, ZFDA, ZARI, Mkemia Mkuu, DPP, Mahakama, Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), UNDP, World Bank, UNEP, GEF, GCF, UNODC, UK- Border Force, British Kingdom, UNFPA, UNICEF, Global Fund, PEPFAR, UNAIDS, Qatar Charity, DEA, Madrasa Earlier Childhood Program, NAD, NOAH, Emarates Lessure, Muzdalifah foundation na Climate Action Network Tanzania. Pia, nazishukuru taasisi zote zisizo za kiserikali zikiwemo ANGOZA, ZACCA, ZAPHA+, PIRO, ZMBF, ORYX COMPANY, MIFF, ZAYEDESA, ZANPUD, ZYF, TFED, zinazofanya, kazi na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na ninawashukuru sana Viongozi wa Dini katika kutusaidia kujenga imani za waumini katika kupambana na dawa za kulevya, maambukizo ya ukimwi, uhifadhi wa mazingira na kuwajali Watu wenye Ulemavu.

90. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nimshukuru kwa dhati Katibu Mkuu Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Bi Maryam Juma Abdalla kwa namna ambavyo ananisaidia kwa karibu sana katika kutekeleza majukumu yangu pamoja na Wakuu wa Taasisi na Idara zote za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wakiwemo Wakurugenzi, Makamishna na wenye viti na wajumbe wote wa Bodi zinazosimamia Taasisi za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa utendaji wao makini. Aidha, kwa upekee ninawashukuru watumishi na watendaji wote wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

91. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho, kwa namna ya kipekee navishukuru sana vyombo vya habari vya Serikali na binafsi kwa kuiunganisha vizuri sana Afisi yetu na jamii. Michango yao imesaidia sana katika kurahisisha utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku.

92. **Mheshimiwa Spika,** Nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimae waidhinishie Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais makusanyo ya mapato ya shilingi Milioni 700,801,000 na fedha za matumizi ya shilingi Bilioni 27,182,108,000 kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa mchanganuo uliotolewa.

93. **Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.**




.................................................


**MHE. HARUSI SAID SULEIMAN (MBM)**
**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS, ZANZIBAR.**

# VIAMBATANISHO


**KIAMBATANISHO NAMBARI 1:** Idadi ya maeneo ya kimazingira yaliyofuatiliwa





**KIAMBATANISHO NAMBARI 2:** Idadi ya vikundi vya watu wenye ulemavu vilivyopatiwa mikopo na wanufaika wa mikopo.




**KIAMBATANISHO NAMBARI 3A:** Idadi ya kesi (za waliokamatwa na dawa) zilizopelekwa mahakamani





**KIAMBATANISHO NAMBARI 3B:** Idadi ya kesi waliokamatwa na dawa zilizohukumiwa




**KIAMBATANISHO NAMBARI 3C:** Thamani ya mali zilizotaifishwa




**KIAMBATANISHO NAMBARI 4:** Idadi ya waraibu waliopatikana katika kituo cha huduma za upataji nafuu



**KIAMBATANISHO NAMBARI 5:** Kiwango cha maambukizo ya VVU



**KIAMBATANISHO NAM.6:** Muhutasari wa Makusanyo ya Mapato kwa kipindi cha Julai 2024- Machi 2025

| Kasma | Aina ya Mapato | Kilichopangwa kwa mwaka (2024/2025) | | Jumla | Kilichopangwa Mwezi kwa tisa (Julai 2024 - Machi 2025) | | Jumla | Kilichokusanywa kwa Mwezi tisa (Julai 2024 - Machi 2025) | | Jumla | % ya miezi tisa | % ya mwaka |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Unguja | Pemba | | Unguja | Pemba | | Unguja | Pemba | | | |
| 1422018 | Uhifadhi wa Mazingira | 313,600,000 | 103,300,000 | **416,900,000** | 235,900,000 | 82,600,000 | **318,500,000** | 162,300,000 | 27,495,000 | **189,795,000** | 46 | 60 |
| 1422019 | Ukaguzi wa Mazingira | 155,000,000 | 48,000,000 | **203,000,000** | 116,000,000 | 36,000,000 | **152,000,000** | 93,500,000 | 21,900,000 | **115,400,000** | 57 | 76 |
| | **JUMLA** | **468,600,000** | **151,300,000** | **619,900,000** | **351,900,000** | **118,600,000** | **470,500,000** | **255,800,000** | **49,395,000** | **305,195,000** | **49** | **65** |

# KIAMBATANISHO NAM. 7A: Muhutasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai 2024 - Machi 2025

| | KILICHOPANGWA | | | | | KILICHOPATIKANA | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU** | **BAJETI YA MWAKA 2024/2025** | **MAKADIRIO MIEZI 9 (JULAI 2024-MACHI 2025)** | **MISHAHARA** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **RUZUKU** | **MISHAHARA** | **%YA MISHAHARA** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **%YA OC** | **RUZUKU** | **%YA RUZUKU** | **JUMLA** | **% YA JUMLA** |
| PB0101: Uratibu wa Mabadiliko ya Tabia ya nchi | 3,145,841,622 | 377,924,355 | 233,317,855 | 144,606,500 | | 252,821,671 | 108 | 28,880,893 | 20 | | | 281,802,564 | 75 |
| PB0102: Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu | 1,279,089,813 | 928,594,224 | 367,533,208 | 344,811,016 | 216,250,000 | 412,632,234 | 112 | 124,920,095 | 36 | 70,668,000 | 33 | 608,220,329 | 65 |
| SB010301: Uongozi wa Rasilimali watu na Uendeshaji | 1,679,095,076 | 1,274,535,717 | 614,796,717 | 659,739,000 | | 495,352,547 | 81 | 192,777,633 | 29 | | | 688,130,180 | 54 |
| SB010302: Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | 355,058,957 | 273,864,895 | 111,772,645 | 162,092,250 | | 100,562,100 | 90 | 33,933,892 | 21 | | | 134,495,992 | 49 |
| SB010303: Uratibu na utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba | 1,059,737,913 | 1,009,021,436 | 450,503,435 | 558,518,001 | | 409,116,244 | 91 | 206,225,333 | 37 | | | 616,441,477 | 61 |
| PB0104: Uratibu wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais | 2,747,561,460 | 937,717,640 | 448,687,640 | 489,030,000 | | 471,681,496 | 105 | 192,624,420 | 39 | | | 664,305,916 | 71 |
| **Jumla B01** | **10,266,384,841** | **4,801,658,267** | **2,226,611,500** | **2,358,796,767** | **216,250,000** | **2,142,166,292** | **96** | **779,562,266** | **33** | **70,668,000** | **33** | **2,992,396,558** | **62** |
| PB0401 na PB0402 : Usimamizi wa Mazingira (B04) | 1,835,300,000 | 1,445,812,999 | 850,050,000 | 595,762,999 | | 729,463,431 | 86 | 327,593,166 | 55 | | | 1,057,056,597 | 73 |
| PC0401 na PC0402 : Udhibiti wa Dawa za | 4,955,000,000 | 1,747,700,000 | 874,275,000 | 885,200,000 | | 680,096,725 | 78 | 441,582,581 | 50 | | | 1,121,679,306 | 64 |

| | KILICHOPANGWA | | | | | KILICHOPATIKANA | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PROGRAMU | BAJETI YA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO MIEZI 9 (JULAI 2024-MACHI 2025) | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | MISHAHARA | %YA MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | %YA OC | RUZUKU | %YA RUZUKU | JUMLA | % YA JUMLA |
| Kulevya (C04) | | | | | | | | | | | | | |
| PC0501 na PC0502 : Uratibu wa muitiko wa Taifa wa UKIMWI (C05) | 2,000,686,000 | 1,336,699,984 | 761,299,992 | 575,399,992 | | 472,445,659 | 62 | 273,746,510 | 48 | | | 746,192,169 | 56 |
| **JUMLA NDOGO (B04+C04+ C05)** | **8,790,986,000** | **5,014,972,983** | **2,485,624,992** | **2,529,347,691** | - | **2,178,579,878** | **88** | **1,616,257,784** | **64** | - | | **3,794,837,662** | 76 |
| **JUMLA KUU** | **19,057,370,841** | **9,816,631,250** | **4,712,236,492** | **4,888,144,758** | **216,250,000** | **4,320,746,170** | **92** | **2,395,720,050** | **49** | **70,668,000** | **33** | **6,787,134,220** | **69** |

**Kiambatanisho nambari 8**: Utekelezaji wa miradi ya maendeleo

**Jina la mradi:** Mradi wa uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mfumo wa ikolojia vijijini – “Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience - EBARR”

**Muda: Miaka mitano (**2018 hadi 2024)

**Mfadhili: UNEP**

**Malengo:** kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini nchini kwa kuimarisha mifumo ikolojia na kuwezesha njia mbadala za kujiongezea kipato.

| Nambari | Shughuli | Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | Kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini nchini kwa kuimarisha mifumo ikolojia na kuwezesha njia mbadala za kujiongezea kipato | Jumla ya mabanda 3 ya kufugia kuku yamejengwa | Ujenzi unaendelea, Bado kuweka milango na kuunga umeme |
| | | Mabanda 2 ya kufugia mbuzi yamejengwa | Ujenzi unaendelea, bado banda moja kukamilika |
| | | Mashine 3 za kutotolea vifaranga (Incubator) | |

| Nambari | Shughuli | Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | zimenunuliwa | |
| | | Mafunzo ya ushoni wa vyerehani na upakasaji yametolewa kwa kaya 77 | Mafunzo yamefanyika kwa awamu ya kwanza ambapo vikundi vitatu vya ushoni wa vyerehani na vikundi vya upakasaji kutoka shehia za Matemwe Kijini, Mbuyutende na Jugakuu vimepatiwa mafunzo |
| | | Ununuzi wa mbuzi 60 wa maziwa unaendelea kufanyika | Mchakato wa ununuzi wa mbuzi uko hatua za mwisho ambapo inasubiriwa taarifa ya tathmini kujulikana mzabuni ili apewe tenda. |
| | | Ununuzi wa kuku 300 wa nyama na 300 mayai unaendelea kufanyika | Ununuzi wa kuku wa mayai 300 na kuku wa nyama 300 utafanyika mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mabanda ya kufugia kuku. |
| | | Ununuzi wa seti 60 vifaa vya kufugia nyuki kwa Shehia tatu Umekamilika, vifaa | |

| Nambari | Shughuli | Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | vimekabidhiwa kwa wahusika | |
| | | Ununuzi wa mbuzi 60 wa maziwa | Ununuzi utafanyika mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mabanda ya kufugia mbuzi. |
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hakuna fedha iliyoombwa kwa sababu mradi uliongezwa muda bila ya fedha na hivyo kwa mwaka huu wa fedha zilitumika fedha zilizoingia mwaka 2023/2024 jumla ya shilingi 234,417,000 Mradi huu umekamilika na unatarajiwa kukabidhiwa Afisi ya Wilaya Kaskazini “A” Unguja | | | |

**Jina la mradi:** Mradi wa kuimarisha mfumo wa maji machafu chake chake, pemba

**Muda: Mwaka mmoja (**2024 - 2025)

**Mfadhili: UNEP**

**Malengo:** Kusafisha maji machafu yanayotoka katika makaazi ya watu kabla ya kuingia katika bahari na kusababisha uchafuzi wa mazingira na viumbe hai viliomo ndani yake.

| Nambari | Shughuli | Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | Kuunganisha nyumba (kaya) katika mfumo wa maji machafu | Jumla ya nyumba (kaya) 147 zimeunganishwa katika mfumo wa maji machafu iliopo msingini Chakechake - Pemba | Baadhi ya nyumba hazija unganishwa kutokana na kutokidhi vigezo vya kuunganishwa katika mfumo |
| | Kupanda majani katika mabwawa ya kusafishia maji machafu | Mita sqare 1950 za eneo la mradi zipo katika hatua | Jumla ya aina tatu za majani zilifanyiwa majaribio ambapo aina mbili tu za majani ndizo zilizoota. Kwa hivyo, zoezi la |

| Nambari | Shughuli | Utekelezaji | Maelezo |
| --- | --- | --- | --- |
| | | za kupandwa majani | ung'oaji wa majani limeshakamilika na kwa sasa kazi ya upandaji rasmi wa majani mabwawa hayo inatarajiwa kuanza. |
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, hakuna fedha iliyoombwa kwa sababu mradi uliongezwa muda bila ya fedha na hivyo kwa mwaka huu wa fedha zilitumika fedha zilizopangwa mwaka 2023/2024 ambazo ni shilingi 173,950,000. Mradi huu umekamilika na unatarajiwa kukabidhiwa Manispaa ya Chakechake Pemba. | | | |

**Jina la mradi: Mradi wa kuirithisha Zanzibar ya kijani**

**Muda: Miaka 5 (**2022 - 2027)

**Mfadhili: SMZ**

**Malengo:** kuhamasisha na kuwawezesha wananchi wote wa Zanzibar na wadau mbali mbali kuelewa umuhimu wa misitu, kuhifadhi miti iliyopo, kupanda na kuikuza miti ili kuimarisha mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadae

| **Nambari** | **Shughuli** | **Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa visima kwa ajili ya kusaidia vitalu vya miti | Jumla ya visima 2 vimechimbwa katika vitalu ya Mwanakombo Unguja na Weni Pemba kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa maji katika vitalu hivyo ambayo yatasaidia umwagiliaji wa miche iliyooteshwa | |
| | Utoaji wa miche kwa jamii | Jumla Miche 14,536 imetolewa wadau mbalimbali wakiwemo vikosi maalum vya SMZ na miche hiyo imepandwa katika maeneo mbalimbali wanayoyasimamia | |
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zimeombwa shilingi 1,500,000,000 na hakuna fedha iliyopatikana. Aidha, zilitumika shilingi 268,322,050 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. | | | |

**Jina la mradi:** Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa mazingira

**Muda: Miaka 5 (**2022 - 2027)

**Mfadhili: SMZ**

**Malengo:** Kuimarisha usimamizi wa mazingira na kupunguza athari za Mabadiliko ya Tabianchi

| **Nambari** | **Shughuli** | **Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa ukuta kuzuia maji ya bahari (chumvi) katika eneo la kisiwa panza – Pemba | Ukuta wenye urefu wa mita 70 katika eneo la kisiwa panza – Pemba umejengwa ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuzuia maji ya chuvi kuvamia maeneo ya kilimo na makaazi.<br><br>Ujenzi wa vyoo Katika Jengo la Ofisi za Idara ya Mazingira liliopo Maruhubi. | |
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zimeombwa shilingi 500,000,00 na kupatikana shilingi 353,902,369. | | | |

**Jina la mradi:** Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya tabia - Pemba

**Muda: Miaka 2 (**2025 - 2027)

**Mfadhili: SMZ**

**Malengo:** Kuimarisha huduma za tiba na marekebisho ya tabia

| Nambari | Shughuli | Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia | Hatua za awali za matayarisho ya ujenzi zimekamilika ikiwemo utayarishaji wa makisio ya ujenzi, tathmini ya kimazingira na kipimo cha udongo katika eneo la ujenzi. Aidha Mkandarasi wa ujenzi huo amepatikana ambae ni JKU chini ya usimamizi wa mshauri elekezi ZBA. | |
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zimeombwa shilingi 2,550,000,000 na kupatikana shilingi 125,039,827. | | | |

**Kiambatanisho 9: Mada za Vipindi vya TV na Redio Vilivyotayarishwa na kurushwa**

| S/N | Unguja |
|---|---|
| | **Vipindi vya TV** |
| 1. | Upandaji wa miti na mazingira |
| 2. | Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani na Usafi wa Mazingira |
| | **Vipindi vya Redio** |
| 1. | Mkakati wa taka |
| 2. | Usimamizi wa Taka |
| 3. | Kipindi cha taka na mazingira kuelekea mvua za vuli |
| 4. | Usimamizi wa Mazingira na Miaka 61 ya Mapinduzi Zanzibar |
| 5. | Uwekezaji wa Mazingira |

## Kiambatanisho 10A: Idadi ya Watumishi wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

| Viwango vya Elimu | Sdt1-F.IV | | cheti | | Stashahada | | Shahada ya juu | | Shahada ya kwanza | | Stashahada ya uzamili | | Shahada ya uzamili | | Shahada ya Uzamivu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F |
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 11 | 3 | 1 | 3 | 1 | 11 | | | 5 | 5 | | | 3 | 2 | | |
| Idara ya Mipango,Sera na Utafiti | | | | | | | | | | 2 | | 1 | 4 | | | |
| Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu | 7 | 6 | 5 | 5 | | | | | 10 | 14 | | | 2 | 2 | | |
| Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Pemba | | 1 | | | | | | | | | 5 | 2 | | | | |
| Idara ya Faragha Pemba | 3 | 1 | 1 | 2 | | | 2 | | 1 | | | | | | | |
| Idara ya Faragha Unguja | 4 | 2 | 4 | 1 | 2 | 1 | | | 3 | | | | 3 | 1 | 1 | |
| Idara ya mazingira (Unguja) | 2 | | 2 | | 3 | 1 | 6 | | 2 | 9 | | | 4 | 3 | 1 | |
| Idara ya Mazingira (Pemba) | 4 | 3 | | | 2 | 3 | | | | 1 | | | 2 | | | |
| Mamlaka ya Mazingira (Unguja) | 10 | 6 | 1 | 3 | 2 | 5 | | | 5 | 6 | | | 5 | | | |

| Viwango vya Elimu | Sdt1-F.IV | | cheti | | Stashahada | | Shahada ya juu | | Shahada ya kwanza | | Stashahada ya uzamili | | Shahada ya uzamili | | Shahada ya Uzamivu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F |
| Mamlaka ya Mazingira (Pemba) | 8 | | 3 | | 3 | 2 | 1 | | 3 | 1 | | | 2 | | | |
| Tume ya Ukimwi (Unguja) | 4 | 2 | 1 | | | 5 | | | 5 | 6 | 1 | | 2 | 3 | | |
| Tume ya Ukimwi (Pemba) | 2 | | | 1 | 1 | 2 | | | 2 | 1 | | | 2 | | | |
| Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Unguja) | 7 | 0 | 2 | 1 | 6 | 7 | 0 | 0 | 11 | 13 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Pemba) | 2 | 0 | 0 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 | 5 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Afisi Kuu Pemba | 2 | 2 | | | 3 | | | | | 1 | 5 | | 1 | | | |
| **Jumla** | **66** | **26** | **20** | **18** | **27** | **37** | **9** | **0** | **52** | **61** | **11** | **4** | **27** | **11** | **2** | **0** |

**Kiambatanisho 10Ꞵ: Stahiki za Wafanyakazi**

| Idara /Taasisi | Malipo baada ya saa za Kazi | Likizo | Ubani | Mafunzo ya Muda Mrefu | Mafunzo ya Muda Mfu |
|---|---|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na utumishi | 15 | 28 | 4 | 5 | 5 |
| Idara ya mipango Sera na utafiti | 5 | 1 | | 1 | - |
| Baraza la Taifa la watu wenye ulemavu Unguja | 6 | 19 | | 6 | 2 |
| Idara ya Faragha Unguja | - | - | | 1 | - |
| Idara ya Mazingira Unguja | 1 | 3 | | 3 | - |
| Mamlaka ya Kuziwia na kupambana na Dawa Za Kulevya Unguja | - | 6 | - | 3 | - |
| Afisi Kuu Pemba | 1 | 16 | - | 8 | 4 |
| **Jumla** | **28** | **73** | **4** | **26** | **11** |

## Kiambatanisho 11: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2025/2026

| Kasma (BO4) | Maelezo | Makadirio | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Unguja | Pemba | Jumla |
| **1422018** | Ada ya Hifadhi ya Mazingira | 346,550,000 | 118,300,000 | 464,850,000 |
| **1422019** | Ada ya Ukaguzi wa Mazingira | 187,950,000 | 48,001,000 | 235,951,000 |
| | Jumla | 534,500,000 | 166,301,000 | 700,801,000 |
| | Asilimia | 76 | 24 | 100 |

**KIAMBATANISHO NAM. 12: MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA FEDHA 2025/2026**

| PROGRAMU | Makadirio ya bajeti kwa mwaka 2025/2026 | Kazi za kawaida | | | | Kazi za Maendelo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku PE | Ruzuku OC | SMZ | Wahisani |
| PB0101: Uratibu wa Mabadiliko ya Tabia ya nchi | 6,837,611,000 | 421,286,000 | 502,889,000 | | | 4,500,000,000 | 1,413,436,000 |
| PB0102: Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu | 1,944,100,000 | | | 650,100,000 | 1,294,000,000 | | |
| PB0103: Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais | 2,955,689,000 | 1,654,305,000 | 1,301,384,000 | | | | |

| PROGRAMU | Makadirio ya bajeti kwa mwaka 2025/2026 | Kazi za kawaida | | | | Kazi za Maendelo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku PE | Ruzuku OC | SMZ | Wahisani |
| PB0104: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais | 1,239,836,000 | 752,709,000 | 487,127,000 | | | | |
| **Jumla B01** | **12,977,236,000** | **2,828,300,000** | **2,291,400,000** | **650,100,000** | **1,294,000,000** | **4,500,000,000** | **1,413,436,000** |
| PB0401 na PB0402 : Usimamizi wa Mazingira (B04) | 3,085,100,000 | 1,196,100,000 | 736,900,000 | | | 1,000,000,000 | 152,100,000 |
| PC0501 na PC0502: Uratibu wa muitiko wa Taifa wa UKIMWI (C05) | 2,379,172,000 | 783,200,000 | 748,311,295 | | | | 847,660,705 |


| PROGRAMU | Makadirio ya bajeti kwa mwaka 2025/2026 | Kazi za kawaida | | | | Kazi za Maendelo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku PE | Ruzuku OC | SMZ | Wahisani |
| PC0401 na PC0402: Udhibiti wa Dawa za Kulevya (C04) | 8,740,600,000 | 2,133,800,000 | 2,106,800,000 | | | 4,500,000,000 | 0.00 |
| **Jumla Taasisi** | **14,204,872,000** | **4,113,100,000** | **3,592,011,295** | **0.00** | **0.00** | **5,500,000,000** | **999,760,705** |
| **JUMLA KUU** | **27,182,108,000** | **6,941,400,000** | **5,883,411,295** | **650,100,000** | **1,294,000,000** | **10,000,000,000** | **2,413,196,705** |

## KIAMBATANISHO NAM. 13: FEDHA ZA MIRADI

| Jina La Mradi | Chanzo cha Fedha | Iliyopangwa 2024/2025 | Iliyopangwa Julai -March 2025 | Iliyopatikana 2024/2025 | % ya iliyopatikana | Makadirio kwa mwaka wa fedha 2025/2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mradi wa kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa jamii za pwani ya Zanzibar - Adaptation Fund | ADAPTATION FUND | 547,084,840 | 547,084,840 | 212,231,120 | 0 | 815,220,000 |
| Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Kitaifa na Kuziwezesha Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi. | WORLD BANK | 0 | | 0 | 0 | 750,315,877 |
| Mchango wa fedha za matumizi kwa program za UKIMWI | UNFPA, UNICEF, UNAIDS & GLOBAL FUND | **0** | | **0** | **0** | 847,660,705 |
| **Jumla Washirika wa Maendeleo** | | **547,084,840** | **547,084,840** | **212,231,120** | 39 | **2,413,196,705** |

| Jina La Mradi | Chanzo cha Fedha | Iliyopangwa 2024/2025 | Iliyopangwa Julai -March 2025 | Iliyopatikana 2024/2025 | % ya iliyopatikana | Makadirio kwa mwaka wa fedha 2025/2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani - SMZ | SMZ | 1,500,000,000 | 1,130,000,000 | 0 | 0 | 1,000,000,000 |
| Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani - SMZ | SMZ | 1,500,000,000 | 1,130,000,000 | 0 | 0 | 1,000,000,000 |
| Kukabiliana Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira | SMZ | 500,000,000 | 500,000,000 | 353,902,369 | 71 | 4,500,000,000 |
| Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia-Pemba | SMZ | 2,550,000,000 | 1,912,500,000 | 125,039,827 | 7 | 4,500,000,000 |
| **Jumla SMZ** | | **6,050,000, 000** | **3,542,500,000** | **478,942,196** | **14** | **10,000,000,000** |
| **Jumla Kuu** | | **6,597,084,840** | **4,089,584,840** | **691,173,316** | **17** | **12,413,196,705** |

## Kiambatanisho Namb 14: MGAWANYO WA FEDHA KIPROGRAMU





Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Othman Masoud Othman akipanda mti aina ya mnazi wakati wa kilele cha Maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Micheweni , Mkoa wa Kaskazini Pemba;Tarehe 205/06/2024



Mwanafunzi wa Chuo Kikuu akipatiwa huduma ya upimaji wa hiyari wa virusi vya UKIMWI kutoka kwa Mtoa huduma wakati wa Kongamano la UKIMWI kwa Wanafunzi wa vyuo vikuu vya Zanzibar lilofanyika katika Ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakili Kikwajuni, Unguja; Tarehe 17/11/2024



Wanafunzi mbali mbali wakishiriki katika mchezo wa kuvuta kamba katika bonanza la Michezo kwa wanafunzi wenye Ulemavu na wasio na Ulemavu lililofanyika katika kiwanja cha michezo ya watoto- Kisakasaka Unguja; Tarehe 20/11/2024



Rais Mstaafu wa awamu ya 6 wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abedi Karume akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Kituo cha tiba na marekebisho ya tabia kilichopo Kidimni,Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini,Unguja:Tarehe 02/01/2025